**MATUMIZI YA TASWIRA KATIKA TAMTHILIA ZA SAID AHMED MOHAMED: *PUNGWA, KIVULI KINAISHI* NA *MASHETANI WAMERUDI***


**NA**

**MUINDE DOMINIC NZILU**


**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2018**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na wala haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.

…………………………………………….. ……...............

**Muinde Dominic Nzilu** **Tarehe**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi kupitia idara ya Kiswahili.

……………………………………………………… …………………….

**Dkt. Evans M. Mbuthia** **Tarehe**

………………………………………………………. ……………………..

**Mwl. Leonard Sanja** **Tarehe**

## TABARUKU

Naitabarukia kazi hii mzazi wangu wa pekee Josphine Muinde kwa kunilea na kunifanya niwe na kiu ya kuelimika ili niweze kufaulu siku za usoni. Namtabarukia pia dada yangu Peninah na mumewe Ngatiri kwa kunishika mkono katika masomo yangu tangu shahada ya kwanza. Nitakumbuka fadhila zao daima.

## SHUKURANI

Kwanza ningependa kutoa shukurani za dhati kwa wasimamizi wangu Dkt. Evans Mbuthia na Mwalimu Leonard Sanja kutokana na mwongozo wao uliojaa busara na ushauri tele ulioniwezesha kuikamilisha kazi hii.

Pili, ningependa kuwashukuru wahadhiri wangu wote walionifundisha katika kozi hii ya uzamili. Wote walikuwa tayari kunipokea kila nilipowahitaji. Ingawa ni vigumu kuwataja wote, sina budi kuwataja baadhi yao ambao lau hawangenishika mkono labda singefikia kiwango hiki. Hao ni pamoja na: Prof P.I Iribemwangi, Prof Kineene wa Mutiso, Prof John Habwe, Prof Mwenda Mbatiah, Prof Rayya Timammy, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Ayub Mukhwana, Dkt. zaja Omboga, Dkt. Jerono miongoni mwa wengine. Ninakiri kwamba Stasnifu hii isingekamilika bila mafunzo na ushauri wenu. Nawashukuru nyote kwa kunielekeza vyema.

Ningependa pia kuwashukuru ndugu zangu Joshua, Japheth na Geoffrey kwa kunihimiza na kusimama nami wakati huu wote. Kwa dada zangu: Serah, Kavutha, Magaret, Nyiva, Mwikali na Kanini nawashukuru sana kwa kunitia moyo wa kuendelea na masomo yangu.

Shukrani zangu pia zimwendee mwalimu mkuu wa shule ya upili ya wavulana ya St. Teresa Bwana Wambugu kwa kunipa fursa ya kuendeleza masomo yangu nikiwa mwalimu katika shule hiyo. Pia nawashukuru wanafunzi wenzangu wote tulioweza kujadiliana nao katika masomo haya kama vile Raymond Owalla, Florence Wambui, Victor Menya, Lilian Ndonye, Claris Chaniro, Nicholas Githinji, Cyrus Thuranira, Rose Munyao, Jackline Otieno, Christine Oyiaro, Peter Muita miongoni mwa wengine. Nyote niliowataja na wale ambao sikuweza kuwataja, Mungu awabariki.

Zaidi ya yote, namshukuru Mola kwa kunipa uwezo, siha nzuri, ari na ukakamavu wa kuendeleza masomo yangu.

# IKISIRI

Mada ya utafiti huu ilikuwa kuchunguza matumizi ya taswira katika tamthilia za *Pungwa, Kivuli Kinaishi* na *Mashetani Wamerudi.* Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza matumizi ya taswira katika tamthilia hizi na kuonyesha dhamira na athari zinazotokana na taswira zenyewe. Utafiti huu ulinuia kujibu maswali yafuatayo: Je, ni aina gani za taswira anazotumia S.A Mohamed katika tamthilia za *Pungwa, Kivuli Kinaishi* na *Mashetani Wamerudi,* Matumizi ya taswira yana athari gani katika tamthilia teule na Je, ni dhamira zipi zinazotokana na matumizi ya tawsira katika tamthilia teule. Nadharia ya umitindo iliyotumiwa katika utafiti huu ilituwekea msingi imara wa kutathmini matumizi ya taswira kama mbinu iliyotumiwa na S.A. Mohamed kuwasilishia maudhui mazito katika tamthilia zake. Kupitia kwa matumizi mufti ya taswira maswala yanayohusu jamii kama vile siasa, uchumi, uozo katika jamii, uongozi mbaya, elimu na mengine mengi yamejadiliwa. Matokeo ya utafiti huu yamethibitishwa kuwa katika sanaa ya uandishi kipengee mahsusi cha lugha kinaweza kutumiwa kama kigezo cha kuainisha kazi za mtunzi binafsi. Mapendekezo yametolewa kuhusu maeneo mengine yanayoweza kufanyiwa utafiti.

## YALIYOMO

UNGAMO ---------- ii
TABARUKU ---------- iii
SHUKURANI ---------- iv
IKISIRI ---------- v
YALIYOMO ---------- vi

**SURA YA KWANZA**

**TASWIRA KATIKA TAMTHILIA ZA *PUNGWA, KIVULI KINAISHI* NA *MASHETANI WAMERUDI***

1.1 Usuli wa mada ---------- 1
1.2 Suala la utafiti ---------- 3
1.3 Malengo ya utafiti ---------- 3
1.4 Maswali ya utafiti ---------- 4
1.6 Sababu za kuchagua mada ---------- 4
1.7 Upeo na mipaka ---------- 4
1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada ---------- 4
1.9 Msingi wa Kinadharia ---------- 9
1.10 Njia za utafiti ---------- 13
1.11 Hitimisho ---------- 14

**SURA YA PILI**

**TASWIRA KATIKA TAMTHILIA ZA *PUNGWA, KIVULI KINAISHI* NA *MASHETANI WAMERUDI***

2.1 Utangulizi ---------- 15
2.2 Tamthilia ya *Pungwa* ---------- 15
2.2.1 Muhtasari wa *Pungwa* ---------- 16
2.3 Taswira katika *Pungwa* ---------- 18
2.3.1 Taswira za Kiishara ---------- 18
2.3.2 Taswira za Kimaelezo ---------- 20
2.3.2.1 Taswira za Mwendo ---------- 20
2.3.2.2 Taswira za Mguso ---------- 21
2.3.2.3 Taswira za Maono ---------- 22
2.3.2.4 Taswira za Joto ---------- 24
2.3.2.5 Taswira za Masikizi ---------- 25

2.4 Tamthilia ya *Kivuli Kinaishi* ------------------------------------------------------------------27
2.4.1 Muhtasari wa *Kivuli Kinaishi* -------------------------------------------------------------27
2.4.2 Taswira katika *Kivuli Kinaishi* ---------------------------------------------------------29
2.4.2.1 Taswira za Kiishara ------------------------------------------------------------29
2.4.2.1.1 Kivuli ------------------------------------------------------------29
2.4.2.1.2 Unga wa ndere ------------------------------------------------------------30
2.4.2.1.3 Unga wa rutuba ------------------------------------------------------------ 31
2.4.2.1.4 Tarakimu saba ------------------------------------------------------------31
2.4.2.1.5 Taswira zinazohusu viungo vya mwili ------------------------------------------32
2.4.2.3 Taswira za Mguso ------------------------------------------------------------34
2.4.2.4 Taswira za Masikizi ------------------------------------------------------------35
2.4.2.5 Taswira ya Joto ------------------------------------------------------------37
2.5.1 Muhtasari wa *Mashetani Wamerudi* ---------------------------------------------------38
2.5.2.2 Taswira za Maono ------------------------------------------------------------43
2.5.2.3 Taswira za Masikizi ------------------------------------------------------------45
2.5.2.4 Taswira za Mguso ------------------------------------------------------------46
2.6 Hitimisho ------------------------------------------------------------46

**SURA YA TATU**

**DHAMIRA NA ATHARI ZINAZOTOKANA NA MTINDO WA MATUMIZI YA TASWIRA KATIKA *PUNGWA, KIVULI KINAISHI* NA *MASHETANI WAMERUDI***

3.1 Utangulizi ------------------------------------------------------------48
3.3 Dhamira na athari za matumizi ya taswira------------------------------------------------- 48
3.3.1 Taswira ya Shetani ------------------------------------------------------------49
3.3.2 Taswira ya kuzunguka Mbuyu ------------------------------------------------------------50
3.3.3 Taswira ya Maandamano na Mauti ------------------------------------------------------51
3.3.4 Taswira ya Makabwela na Makabaila ------------------------------------------------54
3.3.5 Taswira ya Wanamapinduzi------------------------------------------------------------ 56
3.3.6 Taswira ya Mwanamke ------------------------------------------------------------ 58
3.3.7 Taswira ya Askari ------------------------------------------------------------58
3.4 Hitimisho ------------------------------------------------------------60

**SURA YA NNE**

**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

4.1 Utangulizi ---------------------------------------------------------------------------------------62

4.2 Muhtasari wa matokeo ya utafiti ----------------------------------------------------------------62

4.3 Hitimisho ------------------------------------------------------------------------------------------ 66

4.4 Mapendekezo ya utafiti zaidi ------------------------------------------------------------------66

MAREJELEO -------------------------------------------------------------------------------------67

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Usuli wa mada

Waandishi wa kazi mbalimbali za kifasihi wana mitindo mbalimbali ya uwasilishaji wa maudhui katika kazi zao. Baadhi ya waandishi hawa hutumia taswira katika uwasilishaji wa ujumbe wao. Kwa mujibu wa Msokile (1993), taswira ni neno lenye matumizi mbalimbali katika uhakiki wa fasihi.

Kulingana na Njogu na Chimerah (1999), matumizi ya taswira katika kazi za kifasihi na hasa tamthilia humsaidia mhakiki wa fasihi kutambua maana mbalimbali za kazi husika na kuzifasiri kikamilifu. Taswira kwa hivyo ni kipengee ambacho hakiwezi kupuuzwa katika usomaji na uhakiki wa tamthilia.

Aghalabu taswira ni mbinu ya kiubunifu ambayo hutumiwa kupitisha ujumbe kwa njia ya kiufundiyenye kufumba maana. Mwandishi hulazimika kuitumia taswira hasa anapozungumzia masuala nyeti na tata yanayoathiri jamii. Taswira aghalabu hutumiwa ili kuchukuana na mazingira na wakati. Waandishi wengi wa kazi za kifasihi hasa tamthilia hutumia taswira ili kuongezea ladha kazi zao na kuzifanya ziwe na mvuto zaidi kwa wasomaji.

Mwandishi wa kazi yoyote ya kifasihi hutekeleza jukumu la kumzindua msomaji kutokana na masuala yanayomwathiri katika maisha. Huwa na jinsi ya kufanya hivyo kwa kutumia mbinu mwafaka ikiwemo mbinu ya kuandika.Waandishi wengi akiwemo Said Ahmed Mohamed wanazungumzia masuala ibuka na nyeti katika jamii. Mbali na uteuzi wa njia mwafaka ya uwasilishaji wa mawazo, mbinu ambazo mwandishi hutumia huweza kumbainisha yeye na kazi zake. Mbinu hizi pia humchorea msomaji taswira kamili ya jamii ya mwandishi na kuonyesha ni kwa nini anaizungumzia jinsi anavyofanya.

Taswira ni mbinu inayotumiwa kuwasilisha ujumbe maalumu kwa njia ya kimafumbo. Ujumbe huu huhitaji ufasiri ili umfikie msomaji kwa njia wazi. Uhakiki wa matumizi ya taswira itakuwa njia mojawapo ya kumsaidia msomaji kuuelewa ujumbe barabara. Matumizi ya taswira hulenga kuibua masuala muhimu, nyeti na tata kama vile ya kisiasa, kidini, kiuchumi na kijamii. Taswira humfikirisha msomaji kwa kumfanya ahusianishe taswira yenyewe na tabia, mambo na vitu mbalimbali

vinavyojitokeza katika maisha yake. Mohamed alitumia mbinu za lugha hususan taswira ili kupitisha maudhui mazito yenye kuangazia masuala nyeti kama vile ya kisiasa, kijamii, kidini na kiuchumi miongoni mwa masuala mengine. Kwa kutumia taswira, Mohamed analenga kuwasilisha ujumbe wake kwa njia wazi zaidi kwa msomaji. Mwandishi huyu anatumia lugha kama chombo na silaha ya kuwasilishia ujumbe wake. Kama asemavyo Senkoro (1988), maudhui hufanywa kuwa muhimu kutokana na namna ya uwasilishaji wake kupitia mbinu za lugha.

Utafiti huu ulichunguza matumizi ya taswira katika tamthilia tatu za S.A. Mohamed: *Pungwa, Kivuli Kinaishi* na *Mashetani Wamerudi*. Uchunguzi wa kiwango cha matumizi ya taswira ulituwezesha kutathmini upekee wa mwandishi wa tamthilia hizi. Kila mwandishi wa kazi yoyote ya kifasihi huwa na mbinu yake teule ambayo amezoea kuitumia ili kuyawisilisha masuala ya kazi yake kwa njia anayoiona bora zaidi. S.A Mohamed anajulikana sana kwa uzoefu wake wa matumizi ya lugha ya kitamathali katika kazi zake nyingi zikiwemo Tamthilia, Riwaya, Mashairi na Hadithi fupi. Baadhi ya kazi hizi zinazojulikana kwa matumizi yake ya lugha ya kimafumbo ni kama: Maua ya Porini, Chui wa kufuga, Jani la Ukoka na Sisimizi Sisi kutoka diwani ya *Sikate Tamaa*, *Amezidi, Asali Chungu* na *Dunia Mti Mkavu.*

Mwandishi yeyote ni sharti ateue mbinu ya lugha inayochukuana na wakati na mazingira anapoandika kazi ya fasihi. Mohamed alipokuwa akiandika tamthilia zake za mwanzo hakukuwa na uhuru wa kuukosoa uongozi. Kwa hivyo uandishi wake ulihitaji kuwa na ustadi mkubwa wa kiuandishi ili kuzuia kukashifiwa na serikali au hata kufungwa jela. Waandishi wenzake kama vile Ngugi wa Thiong'o, Alamin Mazrui miongoni mwa wengine walitiwa kizuizini kutokana na maandishi yao yaliyokosoa serikali. Kutokana na maudhui mazito yanayoangaziwa kwenye tamthilia za S.A Mohamed, mbinu ya taswira imetumiwa kama chombo cha kuwasilishia maudhui. Tamthilia hizi zinafanana kwa kiasi kikubwa kwa kujihusisha na maudhui ya siasa, utabaka, uchumi, uozo katika jamii miongoni mwa masuala mengine.

Kulingana na Njogu na Chimerah (1999), mwandishi hawezi kujitenga na matukio ya jamii yake kwa sababu ana maslahi katika jamii hiyo. Kutokana na kauli hii, ni dhahiri kwamba Mohamed anaathiriwa sana na sera zilizo nchini mwake. Pia tunaweza kusema kwamba tamthilia za *Pungwa, Kivuli Kinaishi* na *Mashetani Wamerudi* zinaonyesha msimamo fulani maalumu wa mwandishi S.A Mohamed.

Utafiti huu uliteua kuchunguza taswira ili kuweka wazi aina za taswira, matumizi ya taswira na athari zinazotokana na taswira zenyewe kwenye tamthilia tulizoteua. Athari kama hizi huenda zilichangia uandishi wa tamthilia hizi. Ukweli wa kauli hii ulitolewa na utafiti huu ulioongozwa na nadharia ya umtindo ili kudhibitisha iwapo yaliyoandikwa katika tamthilia hizi ni kielelezo cha maisha ya jamii halisi ijapokuwa yapo kwenye ulimwengu wa kubuni wa mwandishi na iwapo taswira ilikuwa mbinu mwafaka ya kuyawasilisha.

### 1.2 Suala la utafiti

Utafiti huu ulishughulikia uhakiki wa fasihi kimtindo hasa taswira katika tamthilia. Umeonyesha ni kwa nini taswira ni njia mwafaka ya uwasilishaji wa maudhui mazito katika tamthilia za *Pungwa, Kivuli Kinaishi na Mashetani Wamerudi*. Suala hili ni muhimu kushughulikiwa kwa vile mwaandishi S.A Mohamed ametumia lugha yenye ubunifu mwingi wa kimafumbo usiozoeleka katika tamthilia nyingi. Uandishi wa aina hii unahitaji kufanyiwa uchunguzi wa kina ili kubainisha mwelekeo wa mtunzi huyu. Kuna tofauti kati ya yale yanayoelezwa kwa njia ya moja kwa moja na yale ambayo yameelezwa kimafumbo lakini yanayotoa athari kubwa kwa wasomaji. Kutokana na jambo hili, tunadhamiria kuchunguza dhana ya taswira, dhamira na athari zinazotokana na taswira zenyewe katika tamthilia za *Pungwa, Kivuli Kinaishi* na *Mashetani Wamerudi*.

### 1.3 Malengo ya utafiti

Utafiti wetu unanuia kutimiza malengo yafuatayo:

(i) Kueleza aina za taswira zinazotumiwa na S.A Mohamed katika tamthilia za *Pungwa, Kivuli Kinaishi* na *Mashetani Wamerudi*.

(ii) Kuchambua athari zinazotokana na matumizi ya taswira katika tamthilia teule.

(iii) Kufafanua dhamira zinazotokana na matumizi ya taswira katika tamthilia teule.

### 1.4 Maswali ya utafiti

Utafiti huu unajibu maswali yafuatayo:

(i) Je, ni aina gani za taswira anazotumiwa S.A Mohamed katika tamthilia za *Pungwa, Kivuli Kinaishi* na *Mashetani Wamerudi?*

(ii) Matumizi ya taswira yana athari gani katika tamthilia teule?

(iii)Je, ni dhamira zipi zinazotokana na matumizi ya taswira katika tamthilia teule?

### 1.6 Sababu za kuchagua mada

Tumeamua kushughulika mada hii kwa sababu S.A Mohamed ametumia mtindo wa kipekee katika uandishi wa tamthilia zake. Jinsi ambavyo ameteua na kutumia lugha katika utunzi wake ameathiri mielekeo ya wasomaji wa kazi zake. Lengo kuu la kuchagua mada hii ni msukumo wa kutaka kujua ni kwa nini S.A Mohamed aliamua kuteua taswira kama mbinu kuu miongoni mwa mbinu zingine za lugha katika tamthilia zake tulizochunguza.

Utafiti huu ulishughulikia taswira kwa sababu ni mbinu inayodhihirika wazi katika tamthilia tulizohakiki. Tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* iliandikwa hivi karibuni na haijafanyiwa utafiti katika mbinu ya taswira. Lengo letu la kuiteua miongoni mwa tamthilia za awali za S.A Mohamed ni kubainisha iwapo mwandishi amedumisha mtindo wake wa kutumia taswira katika kazi zake au kuna mabadiliko yoyote katika uteuzi wa mbinu za uwasilishaji wa ujumbe. Hali hii inatokana na sababu kwamba uhakiki hutegemea historia, mazingira na maendeleo ya kijamii katika kila kipindi kipya cha historia (Hough, 1962).

### 1.7 Upeo na mipaka

Utafiti wetu ulishughulikia taswira katika tamthilia tatu za *Pungwa* (1988), *Kivuli Kinaishi* (1990) na *Mashetani Wamerudi* (2016) zilizoandikwa na S.A Mohamed. Tamthilia hizi ndizo zilizotoa data kuu ambayo tuliichanganua katika utafiti wetu. Tulisoma tamthilia hizi na zingine za mwandishi huyu ili kupata data ya kimsingi kuhusu suala letu la utafiti na mwelekeo wa kinadharia.

### 1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Waandishi mbalimbali wamechangia kuhusu mtindo na matumizi ya lugha katika kazi za kifasihi. Sehemu hii iliangazia baadhi ya tafiti zilizofanywa kuhusu mtindo na matumizi ya taswira katika kazi za awali ili kuonyesha zinavyooana kwa kiasi fulani

na utafiti huu. Kwa kuangalia kazi hizi tulipata upungufu fulani uliotuongezea ari ya kuchunguza matumizi ya taswira katika tamthilia tulizoteua. Mbali na tafiti hizi za tasnifu za vyuo vikuu, tulipitia machapisho mengine kuhusu matumizi ya mbinu za lugha ikiwemo taswira.

Kitsao (1975) katika tasnifu yake ya uzamili, 'A stylistic Approach Adopted for the Study of Written Swahili Prose Texts'.Amefafanua dhana ya elimumtindo na mtindo. Anaeleza namna mtindo hujitokeza katika kazi mbalimbali za kifasihi. Amechunguza namna sifa zinazojirudia za kategoria za maneno na kuonyesha uzoefu wa kutumia kategoria fulani miongoni mwa waandishi fulani. Utafiti wake ulitufaa kwa sababu kazi yetu inahusu matumizi ya taswira kama mtindo anaoutumia S.A Mohamed kuwasilisha ujumbe katika tamthilia zake.

Mohamed (1990) katika jarida la *Mwamko*, alijadili matumizi ya lugha katika kazi za fasihi. Alitoa mifano yake katika mojawapo ya tamthilia tuliyoihakiki ya *Kivuli Kinaishi* (1990). Wakati huo, tamthilia hii ilikuwa mswada wake. Makala yake ilitoa ufafanuzi wa kina kuhusu matumizi ya lugha ikiwemo taswira kama mbinu ya lugha. Maelezo yake yalitufaa katika uhakiki wa tamthilia ya *Kivuli Kinaishi* na zingine mbili tulizoteua kwa kufafanua namna taswira inaweza kutumiwa katika uwasilishaji wa ujumbe.

Miriji (1991) alishughulikia uwasilishaji wa ujumbe katika tamthilia ya *Pungwa*. Utafiti wake ulikuwa wa kimtindo. Utafiti wetu pia ni wa kimtindo. Tulifaidika na uhakiki wa Miriji wa uwasilishaji wa ujumbe katika tamthilia ya *Pungwa* mojawapo ya tamthilia tuliyoichunguza. Utafiti wake ulitupatia msukumo wa kuchunguza matumizi yataswira katika kazi yake.

Momanyi (1991) alihakiki matumizi ya taswira kama kielelezo cha uhalisi katika utenzi wa *Al-Inkishafi*. Katika kazi hiyo, amefafanua taswira zinazojengeka ndani ya tamathali za usemi katika kuonyesha kuanguka kwa mji wa Pate. Alionyesha jinsi taswira zinavyokuzwa ili kupitisha maudhui maalumu. Utafiti wetu ulikaribiana sana na wa Momamyi kwa kuwa ulijikita katika matumizi ya taswira kama mbinu ya kimtindo katika tamthilia za *Pungwa* (1988), *Kivuli Kinaishi* (1990) na *Mashetani Wamerudi* (2016). Isitoshe, utafiti wa Momanyi (1991) ulifaidi utafiti huu kwa sababu umebainisha aina mbili za taswira ambazo ni taswira za mawazo na taswira

zinazojengeka kutokana na tamathali za usemi. Taswira hizi pia zimeshughulikiwa katika utafiti huu.

Mohamed S.A (1995) katika kitabu chake cha *Kunga za Nathari ya Kiswahili:Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi*, anafafanua na kueleza maana ya mtindo na kuonyesha dhana mbalimbali za mtindo kama vile: mtindo kama nyenzo zinazofumbata wazo kuu, mtindo kama mtu mwenyewe, mtindo kama jumla ya tabia za lugha za kikundi au mtu binafsi na mtindo kama kuepuka uzoefu wa ukawaida. Utafiti huu ulionyesha kuwa kazi za kubuni zake S.A Mohamed zinaakisi uhalisia wa maisha ya jamii ya leo. Utafiti huu pia ulichunguza mtindo na kuonyesha dhana mbalimbali za kimtindo. Hata hivyo, utafiti wake ulikuwa muhimu kwetu kwa sababu ulitusaidia kuchunguza jinsi S.A Mohamed amekuzataswira katika uwasilishaji wa maudhui mazito ambayo yamefumbatwa kwenye taswira katika tamthilia zake hasa tulizozichambua.

Musyoka (1996) alihakiki fani katika tamthilia nne za J.Kitsao. Alichambua namna fani ikiwemo taswira hutumiwa kujenga kazi ya kifasihi. Alitathmini umahiri na ubunifu wa mwandishi katika matumizi ya fani kwenye tamthilia zake. Utafiti wa Musyoka unahusiana na utafiti wetu kwa kiasi fulani kwa sababu tafiti zote mbili zinachunguza uteuzi wa maudhui na namna ya kuyawasilisha katika kazi ya fasihi. Musyoka alichunguza vipengee vyote vya fani ilhali sisi tulichunguza kipengee mahususi cha taswira na namna zinavyokuzwa na S.A Mohamed katika utunzi wa tamthilia zake. Tulilinganisha mawazo mbalimbali ya utafiti wa Musyoka na tukaona haja ya kuchunguza taswira kama njia mahususi ya kuwasilisha fikira ili kufanikisha maudhui na kumbainisha mwandishina kazi zake.

Sarara (1997) alishughulikia maudhui katika tamthilia tatu za S.A Mohamed – *Pungwa* (1988), *Kivuli Kinaishi* (1990) na *Amezidi* (1995). Alifafanua mawazo muhimu yanayoikumba jamii ambayo yanajitokeza katika tamthilia hizi. Utafiti wetu unalingana na utafiti wake kwa kiasi fulani kwa sababu sisi tulishughulikia namna maudhui katika tamthilia tatu tulizoteua yanawasilishwa kupitia taswira. Utafiti wake ulikuwa wa kimaudhui lakini wetu ni wa kimtindo. Hata hivyo, hatua ya utafiti wetu ya kuangalia taswira kama njia mwafaka ya kuwasilisha maudhui yanayojitokeza katika tamthilia za S.A Mohamed itakuwa ya manufaa kwa utafiti huu.

Khatibu (1999) aliandika kuhusu tamathali mbalimbali za usemi. Mojawapo ya tamathali ya lugha aliyoieleza ni taswira. Alieleza umuhimu wa fani ikiwemo taswira katika kumwezesha mwandishi kuwasilisha mawazo yakekwa hadhira. Kazi yakeilikuwa muhimu sana kwa utafiti wetu kwani ilituelekeza kufahamu namna taswira inavyotumiwa kujenga maudhui ya kazi ya kifasihi na kutupatia msukumo wa kuangazia kipengee mahususi cha lugha ambacho ni taswira.

Magare (2002) alihakiki mbinu za lugha katika tamthilia ya S.A Mohamed ya *Amezidi* (1995). Mojawapo ya mbinu ya lugha aliyobainisha katika kazi yake ni taswira. Huu ndio msingi wa kazi yetu. Utafiti wa Magare ulitumia tamthilia moja ya S.A Mohamed. Utafiti wetu ulipata msukumo wa kuangazia tamthilia tatu za mwandishi huyu huku ukichunguza taswira pekee. Hata hivyo, utafiti wake ni muhimu sana kwetu kwa sababu yeye ametuwekea msingi wa matumizi ya taswira katika tamthilia za S.A Mohamed.  Kwa sababu tulichunguza tamthilia za mwandishi mmoja, utafiti wake ulitupatia msukumo wa kutaka kujua ikiwa taswira zinazopatika katika tamthilia ya *Amezidi* (1995) zilitumiwa  katika tamthilia za awali za *Pungwa* (1988), *na Kivuli Kinaishi* (1990) au zimetumiwa katika tamthilia ya hivi karibuni ya *Mashetani Wamerudi* (2016).

Nyanchama (2004) alizungumzia matumizi ya taswira katika Diwani ya S*auti ya Dhiki*. Alionyesha jinsi Abdilatif alitumia taswira na ishara katika kuwasilisha maudhui yake. Utafiti wa Nyanchama ulihakiki matumizi ya taswira katika utanzu wa ushairi. Utafiti wetu ulichunguza matumizi ya taswira katika utanzu wa tamthilia. Hata hivyo, utafiti wa Nyanchama ulikuwa muhimu kwetu kwa kuwa ulifafanua matumizi ya taswira kifasihi kazi inayohusiana na utafiti wetu.

Ongarora (2007) alichunguza mtindo katika *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine.* Anafafanua mtindo kama mchanganyiko wa mambo mawili makubwa:wazo (maudhui) la msanii na jinsi wazo hili lilivyoelezwa na msanii. Pia ameangalia mtindo kama tabia ya mtu binafsi au mazoea ya mwandishi ambayo hujitokeza katika matumizi ya lugha. Anasema, ingawa waandishi wa Kiswahili wanatumia lugha ya Kiswahili, kila mwandishi ana mtindo wake wa kuyaeleza masuala anayomulika. Uchunguzi wake wa diwani ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine* umeonyesha namna Said Ahmed Mohamed ametumia mtindo wa kipekee na namna alivyofanikiwa kuwasilisha ujumbe wake na kuacha athari kwa wasomaji kwa kutumia lugha ya

kipekee. Utafiti huu ulitufaa katika kazi yetu ya kutathmini mtindo wa matumizi ya taswira katika tamthilia za S.A Mohamed za *Pungwa, Kivuli Kinaishi* na *Mashetani Wamerudi.*

Musembi (2008) alishughulikia matumizi ya taswira katika riwaya za Mkangi za *Walenisi* na *Mafuta*. Alibainisha jinsi uhalisia unavyodhihirika katika vitabu vya mwandishi huyu kupitia matumizi ya taswira.  Alionyesha kuwa kazi za kubuni za Mkangi zinaakisi ufaafu wa matumizi ya taswira. Uhakiki wake unafanana na wetu ingawaje sisi tulihakiki kazi za mwandishi tofauti.  Hata hivyo, ulitusaidia kupata msukumo wa kuchunguza matumizi ya taswira katika kazi yetu.

Makocha (2010) alichanganua fani ikiwemo taswira katika riwaya ya Said A. Mohamed ya *Kiza katika Nuru*. Alionyesha michakato inayohusika katika upunguzaji wa maana ya neno iliyosimbwa na maana iliyofasiriwa. Amechanganua semi akibainisha jinsi maana kwenye usimbaji kisemantiki hubadilika kutegemea muktadha. Utafiti wake ulitusaidia pakubwa hasa katika mchakato wetu wa kuangalia namna taswira zinaweza kufasiriwa kwa namna tofauti na kutoa athari mabalimbali. Ufasiri mzuri wa lugha inayotumiwa ndio hufanikisha maudhui. Hivyo basi, kazi yake ilikuwa muhimu kwetu kwani ilitupatia mwelekeo wa kuchunguza maana inayolengwa na Said Ahmed Mohamed katika uwasilishaji wa maudhui kwa kutumia taswira katika tamthilia zake tulizozichunguza.

Ngunjiri (2010) alishughulikia matumizi ya taswira kama kigezo cha kufanikisha maudhui katika *Utendi wa Siraji*. Alifafanua matumizi ya taswira katika utenzi huu. Utafiti wake ni wa upimaji wa kimtindo. Utafiti wake ulishughulikia taswira sawa na utafiti wetu. Ingawa alitumia utenzi kwenye uhakiki wake, alionyeshanamna taswirailitumiwa katika kazi hiyo. Utafiti wake unalandana na wetu kwa kiasi fulani kwa kuchunguza mbinu moja ya lugha ambayo ni taswira.

Mirikau (2011) alihakiki matumizi ya taswira ya mwanamke katika tamthilia za Wamitila. Katika utafiti wake alifafanua dhana ya taswira kama jinsi mtu au kitu kinavyochora picha na kuitoa picha hiyo wazi kwa namna inavyoonekana. Mtazamo wake wa picha ni kuwa picha huundwa kwa mafikira ya kiakili ya binadamu.Kulingana naye, picha hudhihirika kutokana na matendo binadamu

anayotenda au kutendewa. Utafiti wake ulikuwa wa manufaa sana kwetu hasa ikizingatiwa kwamba alifafanua suala la taswira. Tulilinganisha mtazamo aliouchukua kuhusu dhana ya taswira na ambao utafiti wetu ulichukua ili kufanikisha matokeo kwa njia bora.

Taswira ni mbinu mojawapo ya tamathali za usemi na hutumiwa kuwasilisha ujumbe uliofumbwa. Matumizi ya taswira huchochewa na mabadiliko ya wakati, mazingira na masuala yanayoathiri jamii. Wamitila (2003) anaeleza taswira kama picha zinazotokana na maelezo ya mwandishi ya moja kwa moja au picha ambazo zinatoa maelezo ya ziada. Kulingana naye, taswira zinaweza kuwa za aina mbili: taswira za kimaelezo na taswira za kiishara. Anaeleza kwamba msingi wa matumizi ya taswira ni kuweza kuchochea hisia mbalimbali ili ujumbe umfikie msomaji kwa nguvu zaidi na uwe na mvuto mkubwa kisanaa.

Msimamo wa Wamitila (2003) kuhusu taswira ni wa muhimu kwa utafiti huu kwani mwandishi S.A Mohamed anawasilisha ujumbe kwa njia ya kumchorea picha msomaji kwa jinsi mbalimbali.

**1.9 Msingi wa Kinadharia**

Utafiti wetu uliongozwa na Nadharia ya Umitindo. Katika ujumla wake, neno mtindo hutumiwa kurejelea jinsi lugha inavyotumiwa katika muktadha fulani na kwa lengo fulani. (Leech na Short 1981)

Maelezo haya yanalingana na yale ya mwanaisimu Ferdinand De Sassure aliyetofautisha dhana ya ujumlalugha na upekeelugha (Langue na Parole). De Sassure alifafanua 'Langue' kama utaratibu mzima wa kanuni za lugha zinazojulikana na wazungumzaji wa lugha husika yaani mfumo wa lugha ya jamii inayohusika. 'Parole' ni matumizi ya utaratibu wa lugha ya mzungumzaji binafsi na pia uteuzi wa kanuni ambazo msemaji huzitumia katika uandishi na uzungumzi wake. Kwa hivyo, mtindo unahusishwa na lugha iliyoandikwa, lugha ya kifasihi na isiyokuwa ya kifasihi.

Katika uandishi wa fasihi, mtindo hutumiwa kwa maana nyingi. Crystal na Davy (1969:1) wamefafanua neno mtindo katika mitazamo minne ifuatayo:

(i) Tabia ya mtu katika matumizi ya lugha.
(ii) Tabia za kundi la watu katika matumizi ya lugha

(iii) Mtindo wa kiupimaji
(iv) Mtindo kulingana na lugha ya kifasihi.

Enkvist (1992) anasema kuwa mtindo aghalabu ni sehemu ya kipengee cha kiisimu katika muktadha na mazingira ambamo hutokea kwa kuchunguza mtindo wa matini, aghalabu vipengee vingi vya kiisimu hulinganishwa na sifa zinazofanana katika matini nyingine.

Murray (1978) anaeleza mtindo kama jumla ya kila kitu kinachoyafanya maandishi ya mtu kutambulikana. Anaendelea kusema kuwa mtindo ni matokeo ya moja kwa moja ya jinsi mtu anavyojieleza kulingana na ujuzi wake wa kujifunza lugha.

Kitsao (1975) anaeleza mtindo kama ukiushi katika matumizi ya lugha ya kifasihi au isiyo ya kifasihi. Unahusisha ukiushi kutoka kaida za lugha ambazo zimezoeleka au za kimapokeo. Ukiushi huu pia hujitokeza katika matumizi ya rejesta au sajili mbalimbali za lugha.

Utafiti huu ulichukulia dhana ya mtindo kama tabia ya mtu katika matumizi ya lugha na jinsi mtu anavyojieleza kulingana na ujuzi wake wa kujifunza lugha kwa kuongozwa na kaida za lugha ambazo zimezoeleka.

Nadharia ya umitindo ilishughulikiwa na Leech (1965) kwenye tasnifu yake ya uzamili. Leech alihusisha Isimu ya usomaji na lugha ya fasihi. Mtazamo wake uliibua hali ya kutoelewana baina ya wasomi wa Fasihi na wale wa Isimu. Alipendekeza mwafaka utafutwe ili uwashirikishe Wanaisimu na Wanafasihi. Kwa hivyo, wahakiki na wasomi walitofautiana kuhusu uhusiano wa kazi za kifasihi na za kiisimu. Ugomvi huu ulipelekea Leech kuandika kitabu *A Linguistic Guide ofEnglish Poetry (*1969*)* ambamo alishughulikia suala la mtindo katika kuchanganua matini za kifasihi. Leech (1969) alieleza:

(i) Elimumtindo ni uhakiki na fasiri ya matini katika mtazamo wa kiisimu.
(ii) Ni taaluma inayofungamanisha uhakiki wa kifasihi na kiisimu ingawa haijisimamii kivyake.

(iii) Msamiati mpana wa kimsingi wa uhakiki wa kifasihi hususan sitiari, taswira, kinaya, usambamba na jazanda hauwezi kufafanuliwa bila kurejelea dhana ya kiisimu.

Kwa hivyo, kama msingi wa kutumia taaluma za kifasihi na za kiisimu, elimumtindo ni uwanja ambamo masuala haya hushughulikiwa. Utafiti wetu ulijikita kwenye matumizi ya taswira kama ilivyobinafsishwa kwenye kazi za S.A. Mohamed

Nadharia ya elimumtindo hutumiwa sana kuhakiki kazi za kifasihi pamoja na maumbo mengine ya matini zilizoandikwa katika nyanja za matangazo ya biashara, utamaduni, siasa na dini. Umitindo pia hubainisha kanuni ya kuelezea uteuzi mahususi unaofanywa na wahusika katika matumizi yao ya lugha kuhusu mambo ya kijamii, utoaji na upokeaji wa maana, uhakiki wa kidiskosi na wa kifasihi (Leech, 1969).

Elimumtindo ni istilahi inayoweza kutumiwa kubainisha uhusiano uliopo baina ya umbo na athari zake katika kiwango fulani cha lugha. Akizungumzia lugha ya fasihi, Leech anasema kwamba athari za matini yoyote ile huamuliwa kwa kiasi kikubwa na mtindo. Hivyo, mtindo ni njia na jinsi lugha inavyotumiwa katika muktadha kwa kuwa msemaji huchagua jinsi ya kuzungumza.

Kimsingi, nadharia hii ina mwelekeo wa kifani na inadhamiria kuchunguza mtindo wa kinachosemwa (maudhui) na jinsi kinavyosemwa (fani). Nadharia hii ina viwango ambavyo humwezesha mchanganuzi wa matini ya kifasihi kuvizingatia ili kutekeleza uhakiki kwa njia ifaayo. Leech (1969), anaorodhesha aina za ukiushi wa kaida katika mtindo wa kazi ya fasihi. Viwango hivyo ni:

(i) Ukiushi wa kimsamiati
(ii) Ukiushi wa kisarufi
(iii) Ukiushi wa kilahaja
(iv) Ukiushi wa sajili au rejesta
(v) Ukiushi wa kimaandishi
(vi) Ukiushi wa kimapisi
(vii) Ukiushi wa kisemantiki

Simpson (2004), anaorodhesha na kufafanua vipengee vya kimsingi ambavyo vinafaa kuchunguzwa katika kazi za kifasihi na mhakiki ambaye anatumia mwelekeo wa

kihakiki wa mitindo. Vipengee hivyo vilivyofanywa na Simpson vinafafanuliwa na Wamitila (2008) kama: lugha ya kitamathali na mtindo, uteuzi wa mtindo, sarufi na mtindo, itikadi, mtazamo wa mtindo na mbinu za uwasilishaji usemi na mawazo. Utafiti huu ulichukua mwelekeo wa kihakiki wa tamathali za usemi na mitindo na pia mbinu za uwasilishaji usemi na mawazo.

Kulingana na Leech (1969), Simpson (2004) na Wamitila (2008), ni muhimu kuchunguza mambo yafuatayo katika matini kwa kutegemea nadharia ya umitindo.

(i) Kiwango cha maandishi. Mfano: fonetiki na fonolojia
(ii) Kiwango cha umbo. Mfano: leksia, matumizi ya lahaja, sajili
(iii) Kiwango cha sarufi. Mfano: mofolojia na sintaksia
(iv) Kiwango cha kisemantiki
(v) Kiwango cha mazungumzo na mbinu za uwasilishaji usemi na mawazo
(vi) Usimulizi au muundo wa masimulizi
(vii) Itikadi, mtazamo na mtindo

Katika utafiti huu, tumeamua kutumia mhimili wa kiwango cha uwasilishaji usemi na mawazo. Maudhui humfikia anayelengwa vizuri ikiwa yatawasilishwa kwa njia mwafaka inayoafiki ujumbe wenyewe na mpokezi. Huu ndio msingi wa mawasiliano yenyewe. Sifa za matumizi ya tamathali za usemi ikiwemo taswira huwa na athari kubwa katika uchanganuzi wa kazi ya kifasihi.

Mhimili wa pili unatokana na mawazo ya Wamitila (2008) anayeongezea dhana ya udhamiriaji (modality) kama sifa nyingine muhimu katika uchunguzi wa kisarufi. Udhamiriaji ni njia ya kiisimu ya kuelezea nia aliyonayo mtumiaji wa lugha. Kwa hivyo, udhamiriaji unaweza kuwa wa uwezekano, unuiaji, ulazima au umazoea. Mawazo ya Wamitila (2008) kuhusu sarufi na udhamiriaji yalikuwa muhimu sana katika utafiti huu. Maelezo yake kuhusu uteuzi wa sarufi na suala la udhamiriaji ndio ulituwekea msingi thabiti wa utafiti wetu. Hoja yake kwamba udhamiriaji unaweza ukawa wa umazoea ndio imekuwa mhimili mkubwa wa kazi hii. Hili linatokana na malengo ya utafiti wetu wa kuthibitisha umazoea wa mwandishi binafsi wa kutumia taswira katika kazi zake hasa tamthilia.

Kazi ambazo tulishughulikia za *Pungwa, Kivuli Kinaishi* na *Mashetani Wamerudi* zimeandikwa kwa ufundi mkubwa wa kimawazo na wa kiuwasilishaji. Utafiti huu

ulilenga kutoa changamoto kwa waandishi na wasomaji wa fasihi kwa kutilia maanani mtindo wa matumizi ya taswira ili wanaosoma na kuandika wajenge mielekeo ifaayo katika ukuzaji wa maudhui.

Nadharia ya umitindo iliweza kutusaidia kuchanganua taswira na namna zinavyotumiwa na mwandishi kufanikisha ujumbe wa kazi yake. Pili, tumezingatia kwamba kila mtunzi wa kazi ya fasihi huwa na upekee wake wa utunzi unaoweza kumtofautisha na watunzi wengine hata kama wataandika utanzu mmoja na pia katika kipindi kimoja. Kulingana na Leech (1969), kazi ya fasihi hulenga kuwasilisha hisi au tajriba fulani kwa wasomaji. Wanamitindo hushikilia kwamba lugha ndicho chombo muhimu kinachosaidia katika uelewaji wa ujumbe uliokusudiwa na mwandishi. Kwa hivyo, nadharia ya umitindo inashirikisha ujumbe na lugha. Hoja hii inahusiana na utafiti wetu kwani ni kupitia ustadi wa kutumia lugha mathalan taswira ambapo S.A Mohamed ameweza kuyawasilisha maudhui ya kazi zake kwa wasomaji kwa njia bora zaidi.

**1.10 Njia za utafiti**

Utafiti huu ulifanywa kupitia usomaji wa maktabani. Tulisoma kwa kina vitabu, majarida, tasnifu na machapisho mengine yaliyohusiana na mada yetu ya utafiti. Kusoma huku kulituwezesha kujenga msingi bora wa kulifahamu pengo na yaliyoandikwa kuhusu mada yetu. Tulilenga kusoma yale yaliyoandikwa kuhusu mbinu za lugha hasa taswira na matumizi yake katika uwasilishaji wa ujumbe katika kazi za fasihi. Usomi wa maktabani pia ulituwezesha kupata mwelekeo wa kinadharia na kukusanya data zilizotufaa, kuzichanganua na kuwasilisha matokeo yake.

Data ya utafiti huu ilikusanywa kutoka kwa tamthilia za *Pungwa*, *Kivuli Kinaishi* na *Mashetni Wamerudi.* Tulizisoma tamthilia hizi kwa kina na tukatenga mambo yote yaliyo muhimu kwa utafiti huu kwa kuyaandika. Mambo tuliyoyatenga ni pamoja na maudhui na taswira zilizopatikana katika tamthilia hizi. Data iliyopatikana baada ya kukusanywa ilichanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti huu na nadharia iliyotumiwa. Katika uchanganuzi, tulibainisha taswira kama zilivyotumiwa katika tamthilia hizi. Data yote iliyokusanywa iliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Uwasilishaji wake ulizingatia malengo ya utafiti huu kwa misingi ya mihimili ya nadharia ya umitindo. Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kwa njia ya maandishi kinathari.

## 1.11 Hitimisho

Katika sura hii, tumefafanua mada ya utafiti wetu iliyohusu matumizi ya taswira katika tamthilia za S.A Mohamed. Tumejadili pia tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, na sababu za kuchagua mada. Tumejadili pia upeo na mipaka na yaliyoandikwa kuhusu dhana ya taswira ili kushughulikia pengo la utafiti wetu kwa ukamilifu.

Nadharia ya umitindo ni nadharia iliyoongoza utafiti huu kwa uwezo wake wa kutathmini matini yoyote kwa kuangazia mtindo. Mtindo ni njia na jinsi lugha inavyotumiwa katika muktadha kwa kuwa mwandishi huchagua kile anachokiandika na njia ya kukiandika. Kazi hii ilichunguza taswira na jinsi inavyoweza kutumiwa kumbainisha S.A Mohamed na kazi zake hasa za kitamthilia.

# SURA YA PILI

# TASWIRA KATIKA TAMTHILIA ZA *PUNGWA, KIVULI KINAISHI* NA *MASHETANI WAMERUDI*

## 2.1 Utangulizi

Fafanuzi mbalimbali zimetolewa na wasomi na wataalamu tofauti kuhusu dhana ya taswira. Hata hivyo, kila jamii huwa na ufafanuzi wake wa taswira kulingana na mazingira yake. Mabadiliko haya ya kimazingira hutokana na mabadiliko ya hali, vitu mbalimbali na utamaduni unaohusishwa na jamii husika. Jambo hili lina maana kwamba ni sharti taswira zielezwe katika muktadha maalumu.

Lanham (1991) anaeleza taswira kama kitu kinachowakilisha kitu kingine, kiashiria, kibadala cha au matumizi ya kitu cha pili kinachofanana na cha kwanza. Naye Senkoro (1987) anaeleza taswira kama mbinu ya lugha inayotumiwa kuchorea picha kitu au mahali kwa kutumia ishara.

Mulokozi na Kahigi (1973) walifafanua taswira kama picha inayoundwa na matumizi ya lugha katika utunzi mzuri wa maneno wenye kuhusisha dhana mbalimbali zinazoleta athari katika mawazo ya msomaji au msikilizaji.

Welleck na Warren (1982) walieleza taswira kama kitu chochote kinachofanana na kingine, jambo au picha ya kufikiria inayowakilisha kitu bayana. Kulingana na Senkoro (1982), taswira hugawika katika makundi matatu; taswira za mawazo, taswira zionekanazo na taswira za kuhisi. Naye Wamitila (2003) anafafanua makundi mawili makuu ya taswira; taswira za kuashiria na taswira za kimaelezo. Kulingana naye, taswira ni picha inayomjia msomaji akilini anapoisoma kazi fulani ya kifasihi. Picha hizi hujengwa na tamathali za usemi kama vile tashibihi na istiari.

Sura hii imejadili taswira mbili kuu: taswira za kiishara na taswira za kimaelezo. Taswira za kimaelezo zimejumulisha taswira za joto, taswira za mwendo, twasira za mguso na taswira za masikizi.

## 2.2 Tamthilia ya *Pungwa*

Tamthilia ya *Pungwa* ni mojawapo ya tamthilia za awali zake S.A Mohamed. Ni kati ya tamthilia zilizoandikwa kwa ustadi mkubwa huku suala la matumizi ya lugha ya kitamathali likipewa kipaumbele. Mwandishi ametumia tamathali nyingi za lugha kama vile methali, istiari, jazanda, tashibihi, taswira miongoni mwa mbinu nyingine.

Kati ya mbinu hizi za lugha, taswira ni mbinu inayoonekana kutawala katika tamthilia hii.

### 2.2.1 Muhtasari wa *Pungwa*

Tamthilia ya *Pungwa* imeandikwa kwa njia ya kipekee isiyo ya moja kwa moja ili kuwasilisha masuala mazito yanayokabili jamii. Masuala haya yameangaziwa katika sehemu sita. Kuna kitangulizi cha kisa ambapo sauti ya kutisha inasikika. Mwandishi ametumia sauti hii ili kuonyesha namna Ukoloni Mkongwe ulivyokidhiri kwenye mataifa ya ulimwengu wa tatu. Kwa Mfano tunaelezwa:

> Sauti ya mzuka: Mimi mzuka wa wazuka,
> Mimi pepo wa mapepo,
> Mimi jini wa majini,
> Mimi wa ardhini na wa baharini,
>
> Mimi niwezaye ruka angani,
> Mimi niwezaye tua ardhini,
> Mimi niwezaye kupasua ardhi na
> kuzama na kuibuka(Uk.3-4)

Katika sehemu ya kwanza, mwandishi anaendeleza maudhui ya Ukoloni Mkongwe. Mhusika Bwana anaonekana mwenye wasiwasi mwingi wa kuhofia kupokonywa mamlaka. Anaishi kwa kuota ndoto hali inayomuudhi Bibiye. Anasema:

> Bwana*:* Mimi kila siku naoteshwa ndoto mbaya. Sijui mara kuna dhoruba, mara kuna tetemeko la ardhi, mara tumegharikishwa, mara… (Uk.8)

Wasiwasi huu wa Bwana unamfanya aonekane kama mgonjwa wa akili. Bibiye anamtafutia daktari wa kienyeji (Bwana mahoka) ili autibu ugonjwa wake.

Katika sehemu ya pili Mahoka anajaribu kuutibu ugonjwa wa Bwana lakini anashindwa. Hata hivyo anatarajia malipo mazuri kutoka kwa familia hii ya kikabaila. Isitoshe anatilia shaka malipo yake. Mfano anasema,

> Mahoka: Sisi hufanya vyema mara nyingi bila kutarajia malipo, lakini kwa maskini wenzetu. Matajiri ndio matajiri tena, lazima mtulipe. Tena…malipo halali (Uk 13)

Maneno haya ya Mahoka yanakuza maudhui ya utabaka. Bwana pia anaukejeli uwezo wa Mahoka kwa kusema maneno yafuatayo:

Bwana: Mahoka hajui hata umaskini wake. Na ende tu mimi mzima.
Kwanza mimi na mahoka hatukai baraza (Uk.14)

Katika sehemu ya tatu, Bibiye na Bwana wanagutushwa na sauti usiku wakiwa wamelala. Sauti inakejeli mwendo na tabia zao. Inawadokezea chanzo cha matatizo yanayowakumba. Inawakashifu kwa kwenda kinyume na utamaduni wa nchi yao wenyewe na kubadili mwenendo kwa kuiga ule wanchi za magharibi. Msanii anasema;

Sauti: Nilining'iniza mizani ya jadi itinge sawa,
Mashambani, vijijini na mijini
Hamkutaka kunisikiliza
Nilitaka mning'inie hewani,
Msiwe huku wala kule: mfumbe macho yenu,
Mzibe na masikio yenu,
Mkinge na nadhari zenu zisielekee Kaskazi
Wala Kusi, Mashariki wala Magharibi…hamkutaka……..
Tazameni nyinyi mlivyo mmejaa pupa!
Wazee wetu hawakuwa wakiishi hivi.
Waliishi peponi…walipendana…walishirikiana, walitimka
pamoja wakafurahi pamoja
Tuseme nini? Shetani katukojolea?
Shetani kamkojolea shetani,
Au tumekosea tangu mwanzo kwamba tusingeweza kunin'ginia
hewani.… (Uk. 20)

Katika sehemu hii pia kuna mapambano dhidi ya Ukoloni Mkongwe na Ukoloni Mamboleo. Kila uongozi unapigania nafasi katika utawala. Ukoloni mkongwe unawakilishwa na pepo huku Bwana akiwakilisha Ukoloni Mamboleo. Mvutano huu unadhihirika kwenye mawazo ya bwana alipokuwa akimweleza Bibiye kuhusu ugonjwa uliomkumba. Bwana anajipata kwenye njia panda. Anajitahidi kuonyesha uwezo wake lakini anadhibitiwa na utawala wa kigeni. Tunaelezwa:

Bibiye: nazungumza na nani basi?
Bwana: pepo.
Bibiye: pepo gani? Yule Yule aliyevuka bahari saba na …
Bwana: hata sasa unazungumza na pepo wa kikwetu. Pepo wa kienyeji.
Bibiye: pepo. Pepo wawili sasa; wa kigeni na kienyeji.
Bwana:Nimechotwa akili na pepo wawili sasa, yule wa kigeni na wa kienyeji. Kila mmoja ana nguvu zake kwa wakati wake…na kiti ni mtu mmoja lakini naonahuyu wa kienyeji kadhibitiwa na huyu wa kigeni mara nyingi…(Uk. 24)

Katika sehemu ya nne, Bibiye anatafutia mumewe mganga (Burhani) ambaye anajaribu kumtibu Bwana lakini anashindwa. Badala yake shetani anampunga mganga badala ya mganga kumpunga yeye (Uk 32).

Sehemu ya tano inaonyesha ugonjwa wa Bwana ukizidi. Anaongea na kupiga kelele peke yake. Anawaona watu wakimzunguka wakitaka kumng'oa mamlakani. Anaeleza dhuluma alizowafanyia watu muda huu wote. Anajuta. Anaona akivamiwa na nyoka.
Katika sura ya sita Bwana na Bibiye walivamiwa na wananchi huku wakitaka kuwang'oa mamlakani. Kwa ushirikiano wanafaulu kuukomesha udhalimu wa Bwana na Bibiye na kuwafanya waishi maisha wanaoishi wananchi wa kawaida.

### 2.3 Taswira katika *Pungwa*

Katika tamthilia ya *Pungwa* tulichunguza taswira za aina mbili kuu ambazo ni: taswira za kiishara na taswira za kimaelezo zinazojumulisha taswira za mwendo, taswira za mguso, taswira za maono, taswira za joto na taswira za masikizi.

#### 2.3.1 Taswira za Kiishara

Kwa mujibu wa Leech (1969), taswira za kiishara hutokea akilini mwa msomaji anapoisoma kazi ya kifasihi. Mchakato huu wa kiakili huchangiwa za uteuzi wa lugha wa mwandishi wakati wa kuisuka kazi yake. Leech analinganisha taswira hizi na vitu vinavyotumiwa kwa niaba ya vitu vingine na kutumiwa kutoa ujumbe uliofichika au wa ziada.

Katika tamthilia ya *Pungwa,* utafiti huu umechukulia taswira za kiishara kama picha maalumu inayoundwa kwenye akili ya msomaji ambayo ina ujumbe uliosimbwa. Ujumbe huu unahitaji kufasiriwa kwa njia wazi ili ubainike ipasavyo.

Katika tamthilia hii dawa anazopewa Bwana na Bibiye ni ishara ya mbinu zinazotumiwa na wakoloni ili kuwazuia wenyeji wasilete ushindani. Wageni wanawataka wenyeji wasifahamu kilicho na umuhimu na manufaa kwao. Hata wenyeji kilicho chao wanakiona duni na kisichofaa. Kwa mfano tunaelezwa jinsi Bwana alivyomwambia Bibiye yafuatayo kuhusu dawa za kigeni:

> Bwana: Sitaki kulala usingizi wa Daima. Mimi si mwendawazimu eti, nimewezwakwa mawazo tu…na pia dawa za hospitali zimenichosha. Mnanipa vidonge vya usingizi kama mgonjwa wa

wazimu? Wala sipati nafuu. A-a, sitaki dawa za
kizungu mimi, nataka dawa za kikwetu.(Uk. 6)

Kauli hii inaashiria jinsi Bwana anaonekana kuelewa tatizo linalomkumba lakini Bibiye halifahamu. Kulingana na Bibiye kilicho cha mzungu hakiwezi kupuuzwa. Anadai kwamba dunia ya kale imepitwa na wakati na kwamba manufaa yao binafsi ndio muhimu. Anasema hivi katika nukuu ifuatayo:

Bibiye: Hapo ndipo unapokosea, na ndipo unapodhili
Nafsi yako na yangu; kudhani kwamba
dawa ya hospitali unaweza kuikataa; kudhani
kwamba cha mzungu kinaweza kupuuzwa.
Mimi naishi katika dhahiri ya mambo. Naishi
leo, sio kesho wala jana. Naishi maisha ya rutuba,
chakula na maji kujineemesha.(Uk 6-7)

Katika harakati za Mahoka za kujiandaa kumganga Bwana, kuna uwezekano kwamba anauelewa ugonjwa wake barabara. Anadai kwamba pepo ameifanya akili yake kiti chake. Ana kiaga kwake. Ana deni kwake na ana makubaliano. Watu wake wanamsumbua ili awache kumridhi pepo huyo, lakini hawezi. Bwana anakeketwa na maneno haya na kutoa kilio chake kwa bibiye akisema anaona wingu likimgubika kichwani. Wimbi likimwingia nyumbani huku mkewe akiliruhusu yeye. Baada ya madai ya Bwana, sauti inasikika ambayo haijulikani inakotoka ikisema:

Sauti: Muwele wangu, huyu mumeo, naona anataka
kubawibiwa na kuliwa akili. Kiti changu,kiti
changu bibiye, kihifadhi kisichukuliwe. Kihifadhi
kisije kikakaliwa. Mkinihifadhi nitakuhifadhini.
Sote tuwe wahifadhina; wenye kuhifadhiana na
kusaidiana.(Uk. 15)

Maneno ya Bwana kwamba anaona wingu jeusi na wimbi likimgumbika ni ya kiishara. Katika jamii nyingi za kiafrika kila mara wingu jeusi likitanda linaashiria mvua kubwa ya gharika. Wimbi ni sauti ya ngurumo au nuru zinazosafiri hewani. Mwandishi ametumia ishara hizi kumwandaa msomaji kwa matukio magumu yanayomsubiri mhusika. Sauti inayotolewa ya kumtahadharisha Bibiye ahifadhi utawala inathibitisha haya.Katika mojawapo ya ndoto zake Bwana aliona anga jekundu likianza kutawala. Kwa maneno yake anasema hivi:

Bwana: Aaaa, anga… jekundu…
rangi nyekundu…wekundu nini maana yake? Damu? Uhai? Mauti? Nini wekundu? Ugonjwa unaoangamiza? Ah, hakika ni uhai wangu, mimi siwezi kufa, kwa hivyo ni uhai. Ishara ya uhai wangu. Shetani hafi. Shetani huangamiza,nami nitawaangamiza mahasimu zangu niwamalize…ah, hata wewe mke wangu unaanza kuwa hasimu (Uk. 35).

Katika jamii nyingi za kiafrika rangi nyekundu huaminika kuwa ni ishara ya hatari au bahati mbaya. Kwa hivyo maneno ya Bwana yanaashiria namna kuna hatari inayowasubiri yeye na mkewe kutokana na matendo yao ya kuwadhulumu watu wa tabaka la chini au wanaopinga utawala wao.

### 2.3.2 Taswira za Kimaelezo

Hizi ni taswira zinazotokana na ufafanuzi wa maelezo ya mwandishi. Taswira za aina hii huwa hazihitaji ufafanuzi mwingi kwani ujumbe wake huwa haujafichwa (Mbuthia, 2005). Taswira hizi ni zinadhihirika wazi katika tamthilia ya *Pungwa.* Taswira hizi zimedhihirika kwa njia mbalimbali kama vile: taswira za mwendo, taswira za mguso, taswira za maono, taswira za joto na taswira za masikizi.

#### 2.3.2.1 Taswira za Mwendo

Taswira hizi zinahusika na hali ya matembezi. Katika tamthilia hii taswira hii imetumika tu kuonyesha hali fulani ya hofu inayosababishwa na mwendo na matendo ya wakoloni (Shetani). Mwandishi anaeleza namna sauti ya Shetani inasikika ikidhihirisha mwendo wake.

Sauti: Mimi pepo wa mapepo,
Mimi jini wa majini,
Mimi wa ardhini na wa baharini,
Mimi niwezaye ruka angani,
Mimi niwezaye tua ardhini,
Mimi niwezaye kupasua ardhi na kuzama na kuibuka,
Kufumba na kufumbua kama mchezo….(Uk. 4)

Kutokana na kifungu hiki tunaelezwa namna Shetani anaweza kutembea na kudhihirisha uwezo wake katika matembezi hayo. Katika maneno ya Burhani alipokuwa akiufafanua ugonjwa wa Bwana, alieleza kwa kutumia mwendo wa viongozi wa kileo uliojawa na tamaa na ubinafsi. Alisema hivi:

Burhan: Hiki si kiza cha wafu. Si kiza cha watu waliokufa.
Hiki ni kiza cha walio hai. Cha wenye kwenda
na kurudi. Cha wanaokwenda bila ya hadhari ya kutaka
kuona nyuma wanakotoka na mbelewanakokwendea.
Cha wanaokwenda mpaka wajigonge, waanguke ndio
warudi nyuma kuona kwamba wamekosea. (Uk.30).

Mwandishi anatumia taswira hii ya mwendo ili kuchorea msomaji picha ya namna viongozi wanavyotawala bila hata kujali watawaliwa. Anawashauri viongozi wawe na maadili na kushirikiana na watu ili waepuke migogoro.

**2.3.2.2 Taswira za Mguso**

Hizi ni aina za taswira ambazo zinahusisha athari zinazotakana na hisia za kuguswa. Taswira hizi zinapotumiwa na mwandishi, humchorea msomaji hali fulani ya hisia zinazosababishwa na hali ya kushikwa. Mguso huu unaweza ukawa wa moja kwa moja au wa kifikira. Katika tamthilia ya *Pungwa,* mwandishi ametumia taswira hii ili kusisitiza athari inayotokana na mguso. Kwa mfano, anatumia taswira hii kueleza maisha ya Bwana na mahasimu wake. Katika mazungumzo ya Bwana na Bibiye anaeleza namna alivyowashika na kuwaua wote waliomwendea kinyume. Mazungumzo ya Bwana na Bibiye yanadhihirisha wazi athari zinazotokana na kuguswa. Wanaendeleza mazungumzo ifuatavyo:

Bwana: Nambie basi, miaka kumi na nane nyuma,
lilitokea tukio gani muhimu katika maisha yetu?
Bibiye: Ulimdidimiza hasimu yako, akadidimia dididi!
Bwana…na baada ya miaka mitano?
Bibiye: Ulimsagasaga adui yako mkubwa, akasagika
sagasaga kama unga.
Bwana: …na miaka minane baadaye?
Bibiye: ulimzika mpinzani wako kwenye kaburi lenye
kina kirefu kisicho mwisho. (Uk.40-41)

Katika mazungumzo haya mwandishi ametumia taswira ya kugusa ili kudhihirisha ukatili na uovu wa Bwana katika kipindi chake cha utawala. Ananuia kuwachorea wasomaji picha halisi ya viongozi ambao hushindwa kujizuia wanapolewa ulevi wa uongozi na kuishia kuwashika na kuwaangamiza mahasidi wao wa kiutawala.

Baada ya wananchi kushirikiana waliamua kuleta mabadiliko ya utawala katika nchi yao. Mwandishi anafafanua haya kwa kutumia taswira ya mguso. Wananchi waliandaa maandamano yakiongozwa na kiongozi wao Simba. Waliwashika na kwa pamoja wakawalazimisha Bwana na Bibiye kutoka mamlakani. Harakati zao zilifaulu

kwa sababu  Bwana na Bibiye waliona ni heri kuachilia uongozi kuliko kuangamizwa na wananchi waliokuwa na ghadhabu tele. Tunaelezwa:

> Simba: …(Anakibana kichwa cha Bwana na kukibinya barabara)
> Bwana:  Usinibane kichwa … niache …
> Simba:  Sikuachi …sikuachi mpaka ukubali masharti yetu …
> Bwana:  Masharti gani?
> Simba:  Ucheze ngoma tunayocheza sisi.
> Bwana:  Ndiyo nitacheza.(Uk. 54-55)

Msanii anatumia taswira hii ya mguso ili kuwachorea picha halisi viongozi dhalimu kwa kuwaonyesha matokeo ya mtindo wao wa uongozi. Anawashauri waepukane na unyanyasaji wa wananchi kwani wanaweza kushirikiana na kupitia nguvu za umoja wao wanaweza kuwaondoa mamlakani.

**2.3.2.3 Taswira za Maono**

Hizi ni taswira ambazo hutumiwa na mwandishi ili kuchora picha inayoonekana wazi na msomaji. Taswira hizi hunuia kupambanua maudhui kwa njia wazi zaidi. Katika tamthilia ya *Pungwa,* taswira za kuonekana zinajitokeza kwa njia mbalimbali.

Burhani daktari aliyeitwa kumganga Bwana alieleza kuwa anaona pepo kama ndiye aliyemsumbua Bwana. Alitaja jina la pepo kama Mfakamizi. Hii ni hali ya kula kila kitu bila kubakisha. Huenda alitaja jina hili kutokana na namna aliona Bwana amejilimbikizia kila kitu. Anawapokonya wanyonge kidogo walichokuwa nacho. Anajitafutia utajiri kwa njia ambazo si halali. Tunaelezwa:

> Burhan: Nimeona… Ah, Shetani au pepo … pepo ndiye
> AnayekusumbuaBwana. Pepo anayeitwa mfakamizi.
> Lo! Hatari pepo huyu. Hulakila kitu …
> shaba, chuma, makaa, dhahabu, kahawa, karafuu
> katani, karanga (Uk. 29)

Mwandishi wa tamthilia ya *Pungwa* anatumia taswira ya maono ili kutoa picha ya viongozi wenye tamaa na ubinafsi. Anachorea msomaji picha ya viongozi wa jamii ya leo na kumshauri ajitahadharishe dhidi ya kupokonywa kila kitu hata cha thamani ndogo kama makaa na karafuu.

S.A. Mohamed anatumia mhusika Burhani kufafanulia msomaji matatizo ambayo yanawakumba viongozi walio mamlakani. Burhani anatumia uganga wake kuonyesha jinsi Bwana anakumbwa na tatizo la kutoona yaliyo mbele kutokana na tamaa na ubinafsi. Tunaelezwa yafuatayo:

> Burhani: Hasa, kwani huoni wewe kwamba kuna ukungu mbele yake? Kuna pazia la kiza, huoni wewe?
> Bibiye: Pazia hilo kaliweka nani? Huachi uongo?
> Burhani: Pazia la shetani. Limewekwa na shetani na ukungu wake ambao Bwana anaupuuza makusudi au hajui kama upo. (Uk. 30)

Taswira hii ya maono inadhihirisha uwezo wa viongozi wa nchi zilizostawi wa kuwaadaa viongozi wa mataifa yanayoendelea na kuwafanya wasifikirie matakwa ya nchi zao wanazotawala. Wanawanasa kwa vitu vidogo vidogo na kuwafanya wapuuze wananchi wa kawaida. Vitu hivi vidogo vidogo ndivyo vinavyowatia kile mwandishi anachokiita ukungu.

Taswira hizi zinatokana na hali kwamba Burhani alikuwa jirani yake Bwana. Kwa hivyo alimwelewa vizuri. Aliishi karibu na aliona mwenyewe namna alivyotumia mbinu na njia zisizo halali kujilimbikizia mali. Bali na uganga wake alijua tu tatizo lake sawa na mtu mwingine yule kwani watu waliona mwenendo na tabia za Bwana.
Mwandishi anaendelea kukuza taswira ya maono kwa kuangazia hali ya maisha ya Bwana na Bibiye. Anaonyesha jinsi Bwana na Bibiye waliishi kwenye nyumba moja lakini hawakuelewana. Kila mmoja aliifikiria dunia yake. Hali hii inaweza kuthibitishwa na taswira ya maono katika mazungumzo yafuatayo:

> Bwana: Mimi? Aaaaa-a! Mimi? Mimi kizuu? Mimi mzuka? Kizuu na mzuka katika nyumba yangu mwenyewe? Leo mimi fahali naambiwa kizuu na mzuka katika zizi langu mwenyewe?Ah, hata wewe, iii…wewe ninayekuweka katika kiambo changu unanambia hivyo?Labda hofu yako juu yangu imevuka mpaka.
> Bibiye: Mimi nakuona kivuli tu, na mara nyingine huhisi pumzi zako tu. Sijui unaishi au huishi; au kama unaishi kwa siri au dhahiri. (Uk 10)

Bibiye anamwona Bwana kama kivuli kutokana na tabia zake za kuoteshwa na kudai kumilikiwa na shetani. Kutokana na hali hii, Bibiye anamshughulikia kwa kumtafutia waganga wa kumtibu lakini bila mafanikio. Mwandishi ametumia taswira hii ya

maono ili kumchorea msomaji picha ya utengano wa kimawazo uliopo kati ya mume na mke.

#### 2.3.2.4 Taswira za Joto

Hizi ni taswira ambazo zimetumiwa katika tamthilia ya *Pungwa* kuonyesha hali ya joto inayowakumba wahusika na kuwaletea wasiwasi mwingi unaowafanya kukosa utulivu.Taswira hizi zimetumiwa ili kuchora picha ya hali yawasiwasi unaowakumba wahusika na kuwaweka kwenye hali ya kuchanganyikiwa wasijue la kufanya. Katika tamthilia ya *Pungwa*, Bibiye anaonekana mwenye joto jingi linalotokana na wasiwasi wa Bwana kuugua usiku. Anashika hili na lile asijue la kufanya. Anatafuta wa kumsaidia bila mafanikio. Anasema maneno yafuatayo;

> Bibiye:Toba ya Rabi! Sijui nikamwite nani usiku huu?
> Niko peke yangu. Majirani wote wametuhama. Ndugu
> wote hawatupendi. Wenzetu wamekwenda vilabu au
> Night shows au wamejifungia wanatazama TV au
> Video. Na wengine wako mbali nasi. Na ukitoka nje
> usiku huu litakalokufika usilie na mtu… (Uk. 11)

Katika tukio lingine Bibiye anaendeleza wasiwasi kuhusu ugonjwa wa Bwana. Anaonyesha kutofahamu kile kinachomsumbua Bwanake. Anamlinganisha na gogo kwani hawezi chochote. Anajawa na wasiwasi kwani anashindwa ni shetani gani anayemkumba Bwana ambaye hawezi kupungika. Anashangaa namna watu walivyowatenga. Usumbufu huu umemzidishia joto na hata kumpelekea kuomba usaidizi. Mwandishi anasema;

> Bibiye: Na kuna shetani asopungika?
> Sijui amesibiwa na nini? Sijui amekumbwa na
> shetani gani asiyesikia mbuku wala taire.
> Mtazameni anavyohema, anavyohaha,
> Anavyopiga mikambi na kufurukuta. Mtazemeni
> anavyotetemeka kama anayeugua kindigapopo!
> Ah, hata watu wetu leo wametutenga, labda
> kwa sababu na sisi tuliwatenga… hofu imekuwa
> ugonjwa wetu, hofu imetawala.(Uk. 13)

Mwandishi anawafunza wasomaji namna hali ya kutoelewa kiini cha jambo inavyoweza kuleta taharuki na kusababisha hali ya joto mwilini inayoibuliwa na wasiwasi. Wasomaji wa tamthilia hii wanaweza kuamini kuwa katika jamii nyingi wanawake wakati mwingi hujawa na wasiwasi na kuingiwa na joto jingi sana hasa wakati mambo yanapowaharibikia.

#### 2.3.2.5 Taswira za Masikizi

Hizi ni taswira zinazotokana na hisia za kusikia. Taswira hizi zinapotumika wahusika huwa na athari za moja kwa moja au zisizo za moja kwa moja kutokana na sauti mbalimbali zinazoundika kwenye mawazo. Mhusika huhusisha sauti anazosikia na picha fulani.

Katika tamthilia ya *Pungwa* mwandishi ametumia aina hii ya taswira kuelezea hisia mbalimbali. Bibiye anakumbwa na mshtuko mkubwa wakati anasikia sauti za mumewe Bwana ambaye ana ugonjwa usioleweka. Sauti hii inatoa picha maalumu kuhusu ugonjwa wa Bwana. Kwa mfano Bwana anasema maneno yafuatayo:

Bwana:Mimi ni pepo,
Niliyesafiri ng'ambo saba
Kuja hapa kulowea
Nilikuja hapa jana
Ninakuja hapa leo
Na kesho, kesho kutwa, mtondo na mtondogoo
Nitakuja…nitakuja… Nitakuja kila siku…
Nimo ndani ya kichwa cha mwele. (Uk. 9)

Sauti hii inamwacha mke wa Bwana na masikitiko mengi kwani inamchorea picha halisi ya ugonjwa wa mumewe. Bibiye Analia kilio cha uchungu na kuchanganyikiwa na ugonjwa wa mumewe. Mwandishi anataka msomaji afahamu kwamba matatizo yanayowakumba wananchi yanachochewa na viongozi ambao wanadhibitiwa na viongozi wa mataifa yaliyoendelea. Anafaulu kufanya hivi kupitia matumizi ya taswira za masikizi.

Katika tukio lingine sauti ya Bwana inasikika ambayo pia inamtisha mkewe. Ni sauti ambayo inamchorea Bibiye picha ya uwezo wa kile kinachomiliki nafsi ya Bwana. Jambo hili linamshangaza Bibi kwa sababu ya msururu wa matukio yasiokwisha.

Sauti: Mimi ni shupavu,
Sitetereki, sitatetereka,
Sibadiliki, sitabadilika…
Wache, wache waseme watakavyo…
Watasema mchana usiku watalala…
Mimi pepo wa akina nyinyi si akina wao,
Pepo mwenda nchi kavu, bahari sina haja nayo,
Na anga niko mbali nalo,
Nisikieni wenzangu,
Nisaidieni nipigane na pepo wa kigeni,

Iwapo uwezo wangu mdogo.
Watatumaliza hawa…. (Uk. 25)

Sauti hii inaibua hisia za kutamauka. Hapa sauti ya Bwana inatoa picha ya kufungwa kimawazo na kunyimwa huru. Nafsi yake inaonekana kutofurahishwa na harakati za kile anachokiita pepo wa kigeni. Anaomba usaidizi ili apigane naye. Mwandishi ametumia aina hii ya taswira ili kuonyesha namna viongozi wametamaushwa na hali zao za maisha kwani wamefungwa katika minyororo ya wageni na kuongozwa kama vipofu bila hata kuruhusiwa kutoa kauli zao.

Sauti hii inafuatwa na sauti nyingine ambayo inaonyesha kutoridhishwa na sauti ya kwanza. Taswira hii inaashiria hisia za hasira. Sauti inasema;

Sauti: Mimi nd'o mimi,
Siwezekani,
Nimechimba imarakwa nanga,
Iliyochimba hadi ardhini,
Hadi aridhi ya saba,
Wapo wanaojua uhai wangu,
Nao wananilinda ili niwalinde,
Wananitetea ili niwatetee,
Si peke yangu mimi,
Mimi ndio wa mimi,
Wa jadi na wa matambiko,
Wa wahenga, wa mizuka,
Mahasimu wananihujumu,
Wananitafuta,
Wanatangaza kushindwa kwangu,
Eti nimeshindwa,
Hawaoni kwamba ninaishi mwili na roho…(Uk. 26)

Sauti hii inayotolewa inaibua hisia za hasira na kutoridhika. Inatoa picha ya hali ya kujigamba na kujitambulisha kama mwenye uwezo mwingi usiopingwa na yeyote. Hata katika tukio lingine, sauti nyingine inamsihi Bibiye atunze kiti walichokabidhiwa. Inaeleza yafuatayo:

Sauti: Muwele wangu, huyu mumeo naona anataka kubawibiwa
na kuliwa akili. Kiti changu bibiye, kihifadhi kisichukuliwe.
Kihifadhi kisije kikakaliwa. Mkinihifadhi nitakuhifadhini.
Sote tuwe wahifadhina; wenye kuhifadhiana na kusaidiana.
La sivyo, hiari yenu … sitaki mganga mimi, sitaki kupungwa.
(Uk. 15)

Sauti hizi zikifasiriwa vyema utapata kwamba kuna mgogoro unaojitokeza kati ya watawala wenyeji na wale wa kigeni. Mwandishi anatumia taswira ya sauti ili

kumchorea mwandishi taswira wazi ya ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo. Wakoloni hawataki kamwe kuachilia utawala bali wanataka kumiliki na kudhibiti takriban kila kitu hata wakiwa kwao.

Kwa mujibu wa nadharia ya Umitindo, utafiti huu ulibaini kwamba mwandishi S.A Mohamed amechukua mwelekeo maalumu wa matumizi ya taswira kama njia mwafaka ya kuwasilisha ujumbe katika tamthilia ya *Pungwa*. Mawazo yamewasilishwa kwa njia ya kuchorea msomaji taswira mbalimbali ili abainikiwe na hali ilivyo katika maisha yake. Taswira nyingi alizotumia S.A. Mohamed zinadhihirisha kwa kiasi fulani hali ilivyokuwa, ilivyo na inavyokisiwa kuwa katika siku za halafu. Matendo yanayofanywa na wahusika wakuu ambao ni viongozi yanalingana na matendo yanayoendelea katika jamii ya leo. Ni kawaida kuwaona viongozi wakiwa na hulka kama hizi za akina Bwana na Bibiye katika jamii zetu. Kwa mfano viongozi wengi wa nchi za Afrika wanajilimbikizia mali huku halaiki ya wananchi wakiishi kwenye uchochole mkubwa mno. Isitoshe ni kama kwamba awapati ushauri mwafaka kutoka kwa walio karibu nao.

### 2.4 Tamthilia ya *Kivuli Kinaishi*

Tamthilia ya *Kivuli Kinaishi* ni tamthilia iliyoandikwa miaka ya tisini. Sawa na tamthilia zingine za S.A Mohamed, tamthilia hii imesheheni ukwasi mkubwa wa matumizi ya lugha ya kitamathali hasa taswira kwa lengo lake la uwasilishaji wa maudhui mazito kwa wasomaji.

#### 2.4.1 Muhtasari wa *Kivuli Kinaishi*

Katika tamthilia ya *Kivuli Kinaishi* Said A. Mohamed anamulika muhusika Mtolewa akipambana na udhalimu wa uongozi wa Bi Kirembwe. Katika hadithi hii, Bi. Kirembwe ametajwa kama kiongozi mwenye mamlaka makubwa ardhini na mbinguni.

Kwa miaka mingi wananchi wameishi kwa kuonewa, kunyanyaswa na kudhulumiwa na kiongozi huyu katika nchi ya Giningi. Wanateswa kwa sababu ya nguvu na rasilimali zao wenyewe. Mhusika Mtolewa anachorwa katika tamthilia hii kama mwanaharakati wa kimapinduzi dhidi ya Bi. Kirembwe na hata mfumo mzima wa uongozi wa Giningi.

Katika nchi ya Giningi inayoongozwa na Bi. Kirembwe, ubaya na maovu makubwa yametamalaki kotekote. Viongozi ndio wanaoonekana wakiwa mstari wa mbele katika kutekeleza maovu haya. Ufisadi unaonekana kutamalaki katika nchi nzima ya Giningi.

Mtolewa ambaye ndiye mhusika mkuu katika tamthilia anaishi katika mapambano makali dhidi ya mfumo mwovu wa uongozi dhidi ya wananchi. Mtolewa anajitahidi kuingia Giningi lakini anawekewa vikwazo. Anakosa ruhusa ya kuingia katika nchi ya Giningi. Sharti moja la kuruhusiwa kuingia nchi ile afanye mapinduzi aliombwa hongo ya shilingi elfu tano aiache kwenye lango kuu ili aruhusiwe kuingia.

Mwanamapinduzi Mtolewa anatoa kiasi hicho cha pesa na anaingia huko ili kuikomboa jamii iliyokuwa imepata taabu kwa miaka na dahari. Katika Giningi, hongo ilikuwa kosa kubwa lakini kutoitoa kungemnyima ruhusa ya kuingia Giningi na kukomesha harakati ambazo hatimaye ziliikomboa jamii ya Giningi. Jamii hii ilianza kuona nyeupe kama nyeupe na nyeusi kama nyeusi kinyume na hapo awali ambapo rangi hizi zilionekana tofauti.

Mtolewa alishirikiana na wari kuleta mapinduzi katika jamii ya Giningi. Lengo lao kuu lilikuwa kuangusha utawala mwovu wa Bi Kirembwe. Katika harakati za ukombozi, Mtolewa aliwaunganisha wari na kuwakomboa kifikra kwa kuwalisha unga wa rutuba kinyume na unga wandere waliozoeshwa na Bi. Kirembwe.

Kwenye harakati hizo Mtolewa na wari walikamatwa na kuuawa lakini mwamko wa kisiasa ambao walikuwa wameusababisha ulisababisha raia kuchukua hatua za kujikomboa. Kwa mfano, tunaelezwa yafuatayo kupitia sauti za wananchi:

> Sauti:Tunaishi Bi. Kirembwe, sote tunaishi, sote
> tulioangamia…sura zetu zimo ndani
> ya viwiliwili vya watoto wetu.
> Mawazo yetu yamo ndani ya maisha
> na bongo zao. Imani na itikadi imo ndani ya
> maisha yao…tunaishi, ni vivuli vinavyoishi,
> visivyoweza kufa, ni sauti zinazosema
> kimya kimya na hata kwa matamko
> ya wazi….. (Uk.118-119)

Taswira inayotolewa na sauti hii inaashiria kwamba wananchi wametambua haki zao na kuamua kuzilinda hata ikiwa itawagharimu. Wamejua kwamba umoja na ushirikiano ndio silaha ya ukombozi.

Mwandishi anatumia aina hii ya taswira ili kutoa tahadhari kwa viongozi dhidi ya kuwanyanyasa na kuwadhulumu wanaharakati kwani huwa na watu wengine wanaowafuata na wanaoweza kusimama na kulinda haki zao hata kama viongozi wao wataondoka.

### 2.4.2 Taswira katika *Kivuli Kinaishi*

Kwa mujibu wa Senkoro (2011), taswira ni matumizi ya lugha yanayopambanuliwa na uteuzi mzuri wa maneno, ulinganifu na uwazi wa maelezo unaohusisha dhana mbalimbali tofauti zilizo kwenye dhana moja ili kutoa picha na athari maalumu katika mawazo ya msomaji. Katika tamthilia ya *Kivuli Kinaishi* tuna taswira zifuatazo:

#### 2.4.2.1 Taswira za Kiishara

Taswira za kiishara ni zile zinazotumia ishara kuwakilisha jambo fulani. Ishara hizi huhitaji ufasiri wa msomaji ili kufumbua ujumbe uliosimbwa. Taswira za kiishara zilizotumika katika tamthilia ya *Kivuli Kinaishi* ni pamoja na: kivuli, unga wa ndere, unga wa rutuba, tarakimu saba na viungo vya mwili.

##### 2.4.2.1.1 Kivuli

Kivuli kimetumiwa kuashiria ukoloni mamboleo ambao unaathiri jamii nyingi baada ya ukoloni mkongwe kuondoka. Jamii za kiafrika zimeathiriwa pakubwa na utawala wa ukoloni mamboleo ambapo anayetawala haonekani kama vile huwezi kukiona kivuli lakini athari zake zaonekana wazi hata bila yeye kuwepo.Tunaelezwa:

> Bi Kizee: Bi. Kirembwe aliyekufa lakini yu hai na
> mwenye uwezo wake bado. Uwezo wa
> kichawiwenye kujali nafsi yake (kisirisiri)
> na kujali nyinginewakati mmoja. Uwezo wa
> kujigeuza; mara leo nguru,kesho papa,
> leo kasimama huku na kesho kwingine…
> Bi. Kirembwe anasimama kwa nguvu
> za kitisho; anayeongoza kwa ulumbi
> wake wa kusema,anayerehemu na kuangamiza
> kwa ujanja wake uliofichama…(Uk. 82)

Neno kivuli pia limetumiwa na mwandishi kama ishara ya wanamapinduzi wanaotetea haki za wanyonge. Hata baada ya wao kuondoka vizazi vyao vinatumiwa

kuendeleza harakati walizoanzisha za mabadiliko. Mwandishi anafafanua kwa kauli ifuatayo:

> Sauti: … kweli tumekufa, lakini kilichofifia ni kiwiliwili chetu tu,vivuli vyetu vya roho vipo vinaishi na sauti zetu zinasikika kwa wanaotaka kuzisikia. Hatuna shaka siku moja zitageuka wimbi la kuosha uongo na uchafu uliosambaa Giningi … (Uk. 89)

Kama inavyodhihirika katika nukuu, vita dhidi ya Ukoloni Mamboleo huwa zinaendelea kila wakati kwa sababu uovu huu ungalipo.

#### 2.4.2.1.2 Unga wa ndere

Unga wa ndere umetumiwa na mwandishi kama ishara ya kuonyesha itikadi zinazomfanya mtu akubalike katika tabaka tawala na kuiga miiko ya tabaka hilo. Kwa mfano, tunaelezwa:

> Bi. Kirembwe: Aliponizaa mamaangu
> Wakanilea,
> Wakaniengaenga,
> Nikanyonya titi lake,
> Nikanywa uji wa uwele
> Uliochanganywa na unga wa ndere.
> Nikaogeshwa jimbo la majani ya kila aina…kikwayakwaya…
> Hata weni na upupu,
> Dawa ya kuimarisha hisia yangu
> Iwe ya kifalme, iwe isiyoogopa
> Iwe ya kuamua tunayotaka…
> Ndio au sivyo? (Uk. 41-42)

Unga wa ndere ni ishara pia ya masharti yaliyowekwa na jamii za kijadi ili mtu akubalike katika uongozi katika jamii hiyo. Katika jamii nyingi hasa za bara la Afrika, utawasikia viongozi wa jamii fulani wakifanya hafla mbalimbali za kile wanachokitaja kama kutawaza viongozi wao. Viongozi hawa hukabidhiwa silaha mbalimbali kama ishara ya kukubaliwa kuiongoza jamii hiyo. Tunaelezwa:

> Bi. Kirembwe: Inama … piga goti tukurambishe unga wa ndere ilitukugeuze… tukurekebishe pepo wako kichwanialingane na pepo wa Giningi … (Uk. 52)

Mwandishi ametumia taswira ya unga wa ndere ili kumchorea msomaji picha ya namna viongozi wanavyowalazimisha wananchi wa kawaida kuwaunga mkono katika utekelezaji wa uongozi wao mwovu unaomkandamiza mwananchi mwenyewe. Mwananchi analazimika kuiga mambo kikasuku bila hata kuwa na njia badala. Viongozi kama hawa huogopa mabadiliko na huhofia kwamba mambo yakibadilika huenda wakatoka mamlakani iwapo hawataondolewa.Wanataka kila mtu kuiga maovu na kuona mambo kinyume na ilivyodhahiri. Kwa mfano, waliolishwa unga wa ndere walitarajiwa kuona rangi nyeupe kama nyeusi na nyeusi kama nyeupe. Hakuna yeyote alitarajiwa kufahamu nyeupe ni nyeupe na nyeusi ni nyeusi. Hivi ndivyo viongozi wengi wa nchi za Kiafrika walivyokuwa kama vile Kenya, Zimbabwe, Afrika kusini na zingine.

#### 2.4.2.1.3 Unga wa rutuba

Unga wa rutuba umetumiwa na mwandishi kama ishara ya kuonyesha elimu ya kujitambua katika jamii. Pia ni hali ya kutambua nafasi ya mtu na kuwa na uwezo wa kawaelimisha wengine. Katika tamthilia ya *Kivuli Kinaishi,* Mtolewa mwenye uwezo wa kuwaokoa wanaginingi anasema;

> Mtolewa: Niruhusuni nifungue mkebe huu ili nitoe unga
> wa rutuba…usingizi unakwenda na mwako
> unakuja … chembe ndogo ya unga huu itatutoa
> kwenye kiza; utatuonyesha vitu katika uhalisi na
> uyakinifu wake… njooni mmoja mmoja
> nikurambisheni unga wa rutuba … (uk. 112)

Unga wa rutuba umetumiwa na mwandishi kama ishara ya uzinduzi kwa wananchi unaowawezesha kufahamu haki zao. Mwandishi anaeleza jinsi walioula ‘unga wa rutuba’ walivyojielewa na kujiona kama walivyokuwa wajinga kwa kipindi kirefu. Walianza kuona mambo katika uhalisi wake na kuona kama nuru imewajia.

#### 2.4.2.1.4 Tarakimu saba

Katika imani za kidini hasa wakristo, kuna imani kwamba namba saba huashiria ukamilifu wa jambo. Taswira hii inadhihirishwa katika onyesho la nne. Onyesho hili ndilo linalofafanua mhusika Mtolewa aliyekuja kuikomboa jamii ya Giningi akisaidiwa na wari. Mara tu baada ya kuonekana kwa Mtolewa, msanii anatoa picha ya watu kwenye jukwaa wakiwa katika makundi. Kundi mojawapo lina wazee saba waliokuja kumsaliti Bi.Kirembwe na kuleta ukombozi wa Giningi. Kwa hivyo,

kuonekana kwa wazee saba wa Giningi ni ishara ya ukamilifu unaoashiria ushindi wa wanyonge dhidi ya uongozi dhalimu wa Bi. Kirembwe. Mfano tunaelezwa:

> Sauti: Kumbwaya ugoma maarufu wa Giningi, unalia kabla
> pazia kufunguliwa. Nyimbo inakuja na ngoma, inaimbwa
> kwa sauti za kike kwa kiume, za wakubwa kwa wadogo:
> Pazia linafunguliwa kidogokidogo kuwadhihirisha wari
> wanaotaka kuingizwa Giningi (mmoja wao mtolewa)
> wameketi pamoja kike kwa kiume: wa kiume wamevaa
> vinyamkere na wa kike kaniki za kifua. Upande mwingine
> kuna wazee saba wa Giningi wamevaa vizuri, suti na tai:
> Mbele yao kuna vyakula na vinywaji vya kila aina mezani
> upande mmoja kuna kiti cha enzi cha Bi. Kirembwe…pazia
> linafunguliwa lote, wari wanainuka kucheza, kike kwa kiume,
> wakubwa kwa wadogo…wanacheza kama mazuzu… (Uk. 31)

S.A. Mohamed anamwandaa msomaji kisaikolojia kuhusu mabadiliko yanayotarajiwa kwa kutumia ishara ya wazee saba ambao wana nia ya kuung’oa utawala wa Bi. Kirembwe. Kwa kutumia nambari saba, mwandisshi anaonyesha ukamilifu wa jambo hili. Hali hii inatokana na imani za jamii nyingi kwamba nambari saba ni ya ukamilifu. Kwa mfano, jamii nyingi za dini ya kikristo zina amini kwamba Mungu alikamilisha kazi yake siku ya saba. Kwa hivyo, wanaamini nambari ya saba inaashiria ukamilifu.

### 2.4.2.1.5 Taswira zinazohusu viungo vya mwili

Viungo vya mwili ni taswira ya kiishara inayoonyesa wasaidizi wa kutekeleza shughuli za kuongoza katika milki ya uongozi. Kiongozi yeyote hatekelezi majukumu yake bila usaidizi wa watu wengine wanaomzingira. Viungo hivi mwandishi anasema vilianza kumsaliti Bi. Kirembwe. Kwa mfano, Tunaelezwa:

> Macho ya Bi. Kirembwe: Mimi ni shahidi wa maovu yote
> uliyoyatenda ya kudidimiza na
> kuangamiza.
> Mikono ya Bi. Kirembwe: Hata sisi ni mashahidi ulitutumia
> kubiginya.
> Miguu ya Bi. Kirembwe: Na mimi pia nilikuchukua kwenye
> miendo yako ya kichawi ya kuhusudu
> na kuangamiza… (Uk. 128)

Viungo hivi vya mwili wa Bi. Kirembwe ni ishara ya wale watu waliokuwa karibu sana na Bi. Kirembwe kama vile wazee na watangazaji ambao wanamsaliti kutokana

na matendo yake mabaya. Hali hii ilitokea kutokana na vuguvugu la wanamapinduzi kupamba moto.

#### 2.4.2.2 Taswira za Maono

Ni taswira zinazotokana na haja ya mwandishi ya kumchorea msomaji picha ya tukio fulani inayonekana wazi. Maudhui yake hujitokeza wazi kupitia masimulizi yake. Kwa mfano, Mtolewa anaonekana akiwa amejitolea mhanga ili kuwakomboa wari wenzake kifikra kwa kuwalisha unga wa rutuba. Anasema hivi:

> Mtolewa: Hamtoweza kufahamu mpaka niwatoeni
> mzigo mlio nao… hamtatambua mpaka
> nikufumbueni macho na kukuzibueni
> masikio (Uk. 90)

Bi Kirembwe anadhihirisha namna alivyokuwa na uwezo was kuuona na kuusoma undani wa mtangazaji wake. Hakuhitaji kuelezwa chochote ila aliweza kutathmini na kuona tabia za mtangazaji na azma yake. Tunaelezwa:

> Bi kirembwe: Usisahau kwamba mimi naweza
> kusoma undani wako…
> Mtangazaji: Siunaona…uko mbele yako: damu yangu
> safi haijanajisiwa; unga wa ndere unafanya
> kazi… bongo langu safi kama kioo…sina
> Bi. Kirembwe, sina neno mimi
> mtangazaji wako…(Uk.121)

Katika jamii ya Giningi ishara zote zinaonyesha kwamba Bi. Kirembwe ndiye anayestahili kutawala pekee. Amebadili madaraka ya serikali ya Giningi na kujitangaza kama mtawala wa milele. Tunaelezwa :

> Bi. Kirembwe: Mimi ni Bi. Kirembwe nakukumbusheni.
> Mimi ndiye mrithi wa jadi wa Giningi.
> Ndiye mchawi mkuu ndiye mwenye kustahiki
> kukalia kiti hiki…kukikalia daima dawamu (Uk. 71)

Katika jamii hii ya Giningi inaonekana wazi kwamba wanaginingi wananyimwa haki ya kuwachagua viongozi wao wanaotaka kwa kuwa hakuna demokrasia. Bi. Kirembwe ni wazi kwamba ameiteka nyara demokrasia yao.

Watu wa Giningi walifundishwa kusema uongo badala ya ukweli. Pia walilazimishwa kukubali masharti magumu pasi majadiliano yoyote. Hii ndio maana waliuona usiku

kama mchana na mchana kama usiku. Yeyote aliyejionyesha kuwa na hekima ya kutambua vingine alipewa adhabu ya kifo. Kwa mfano mkulima, tabibu na mwalimu waliuawa walipoeleza matatizo yao waziwazi. Vilevile wale wazee watatu waliuawa kwa kwenda kinyume na matakwa ya Bi. Kirembwe hata kama walikuwa na mawazo mazuri ya kuiendeleza Giningi kimaendeleo. Tunaelezwa :

> Wazee watatu: ….tulidhani tutaweza kutoa mchango wetu; tulijisemea tu, tena ndani ya nyoyo zetu kwamba sisi pia tulikuwa na sehemu ya kutaka kuiona Giningi ya namna tofauti kama tunavyofanya (uk. 74)

Kauli hii ni ishara zinazopambanua wazi kutokuwepo na demokrasia katika Giningi. Uongozi wa kidikteta umeendelezwa na Bi. Kirembwe bila woga wowote.

Mwandishi S.A Mohamed anatumia ishara zinazoonekana wazi kuashiria mateso na unyanyasaji dhidi ya wanyonge. Kwa mfano, anaeleza;

> Mwanaginingi 1: Tuliambiwa tutapewa matrekta kuburuga eneo kubwakama tutaishi pamoja. Na sasa tunaishi pamoja; piatuliambiwa tutaletewa mbolea za kizungu. Hatukuletewa…
>
> Mwanaginingi 11: Sivyo hivyo mheshimiwa … pia hakuna vitabu vya kuandikiawala vya kusomea, hakuna chaki za kuandikia na vifaa vingine kama atlasi, rangi … na hata, mabanda ya shule yanaporomoka…(uk. 18-22)

Mwandishi hapa anamjengea msomaji kitendo cha kuona kwa macho yake ya akili. Anaweza kusawiri jinsi wanaginingi walidhulumiwa na kuachwa kwenye uchochole kutokana na ishara za; kunyimwa matrekta ya kulima, kunyimwa mbolea, kukosekana vitabu, chaki, atlasi, rangi na vifaa muhimu shuleni na hata shule zilizojengwa vibaya kuporomoka. Haya ni matendo wazi msomaji anayoweza kuyasawirina kuyaona kwenye macho yake ya ndani.

### 2.4.2.3 Taswira za Mguso

Ni taswira zinazotumiwa kwenye tamthilia ya *Kivuli Kinaishi* kuibua hisia au picha ya kushikwa. Mwandishi anapotumia aina hii ya taswira anamsababishia msomaji kuona picha ya kushikwa kwenye macho yake ya kiakili.

Baada ya wari wa Giningi kulishwa unga wa rutuba, walijitolea kuungana na Mtolewa ili kuikomboa jamii yao. Hata hivyo, haikuwa rahisi kwao kwani walipingwa sana na walinzi wa Giningi na kila waliposhikwa waliteswa na kudhulumiwa. Mwandishi anatoa picha hii kwa maelezo yafuatayo:

> Mlinzi II: Nimekukamata sasa… kwa nini ukaniendesha mbio? Kwa nini unanitimua? Tazama, unaona n'navyohema hivi? Pumzi juujuu, kwa nini? Mmekuwa kama magombe yaliyovunja zizi kwa njaa na kiu ilhali mnashiba? Kwa nini hamtaki kushiba utulivu wa miaka mingi uliopo Giningi? Kwa nini mnaona kiu kwenye maji safi? Nyinyi waharibifu… (Uk. 104)

Mwandishi anatumia maelezo haya kumchorea msomaji taswira ya kushikwa. Anaonyesha jinsi hasira za mlinzi zimefika upeo na zinavyoweza kuleta maangamizi baada ya kuwashika wanaovuruga amani ya miaka mingi kama anavyosema. Wari wanaozinduka wako kwenye hatari ya kuangamizwa baada ya kushikwa.

Mtolewa kiongozi wa wanamapinduzi yuko kwenye hatari ya kuangamizwa na utawala wa Bi. Kirembwe. Hali hii inadhihirika kutokana na jinsi mwandishi anavyochora picha yake baada ya kushikwa. Anaeleza jinsi walinzi sita walivyoingia wakiwa wamemshikilia Mtolewa kitikiti. Hafurukuti! Wari wanapomwona wanapiga kelele (Uk. 105).

Msomaji wa kauli hii atapata picha halisi ya namna walinzi walivyomshika Mtolewa. Hatutarajii mshiko huu uwe wa kirafiki. Hii inatokana na hali kwamba Mtolewa alikuwa hasidi mkubwa wa utawala wa Bi. Kirembwe. Kwa hivyo, alivyoshikwa ni ishara kwamba alipitia maumivu na hali hii ilisababisha wafuasi wake kupiga kelele.

Jamii ya Giningi inaonyesha kunyanyaswa na kudhulumiwa kwa tabaka la chini. Tabaka hili linawakilishwa na wari pamoja na sauti za wahenga walioangamizwa na Bi. Kirembwe. Linaonewa, kunyanyaswa, kudhulumiwa, kukandamizwa na kusingiziwa kila aina ya uovu. Kwa mfano kuuliwa kwa mwalimu, mkulima, tabibu na hata Mtolewa baada ya kushikwa (Uk. 24-25, 114).

#### 2.4.2.4 Taswira za Masikizi

Taswira za maskizi ni taswira zinazotokana na hisia za kusikia (Mbuthia, 2005). Taswira hizi zinapotumiwa katika tamthilia ya *Kivuli Kinaishi* zinazua athari za moja

kwa moja zinazotokana na sauti. Sauti zinazosikika zinachorea msomaji picha fulani kwenye akili yake.

Katika tamthilia ya *Kivuli Kinaishi* mwandishi amekuza aina hii ya taswira kwa njia mbalimbali. Kwa mfano tunaelezwa:

> Sauti nyingi:Tunaishi Bi. Kirembwe, sote tunaishi,
> sote tulioangamia… sura zetu zimo
> ndani yaviwiliwili vya watoto wetu.
> Mawazo yetu yamo ndani ya maisha
> na bongo zao. Imanina itikadi imo
> ndani ya maisha yao… tunaishi, ni
> vivuli vinavyoishi, visivyoweza
> kufa,ni sauti zinazo sema kimya
> kimya na hata kwa matamko ya wazo
> (uk. 118,119)

Sauti hii inaashiria kwamba mawazo yaliyopandwa na wanamapinduzi wakiongozwa na Mtolewa yapo na yanaendelelea kumsumbua Bi. Kirembwe. Sauti hii pia inamwathiri Bi. Kirembwe hadi anaanza kuuona mwisho wake kwa kusalitiwa na viungo vyake vya mwili (uk. 128)

Ishara ya mapinduzi mengine inatokana na sauti za vizazi vipya vinavyoonekana kuendeleza ukombozi. Tunaelezwa:

> Sauti nyingi: Sisi ni vizazi vipya vya Giningi, vizazi vya
> waliodidimizwa….vizazi vyawaliodidimia…
> sisi tuna kinywa kipana…..tuna uwezo
> wa kuamua tunavyotaka…Kuamua
> wenyewe……..kwa maslahi yawote….
> hatutachanizwa tena na uchawi,tunakuja…….
> tunakuja (Uk. 128)

Mwandishi anaonyesha namna uongozi wa kidikteta una mwisho wake kupitia hatua kwa hatua. Kupitia sauti ya Bi Kizee anasema hivi:

> Bi. Kizee: …hatesi mtesa akafululiza: wakati una uamuzi
> wake….sisi huutaka wakati utende sasahivi,
> lakini kanuni zake hazijatimia, iwapo kama
> wengine wasemavyo jipu halijaiva,Katu haiwi
> sasa hivi, lakini halafu kesho, kesho kutwa na
> hata mwakani…(uk. 131)

Kupitia kwa sauti hii mwandishi anaeleza kwamba matendo maovu yana mwisho wake. Yanapoisha hata wenye kuyaendeleza huisha pia. Hii ndio maana tunamwona Bi. Kirembwe akikejeliwa kwa sauti ifuatayo:

> Sauti: Ah, hata wewe Bi Kirembwe leo umegwaya?
> Unatetemeka kama unjukuti unapopeperushwa
> na upepo? Unalia kama mtoto mchanga au mwanamke
> aliyefiwa na mumewe? Unahofu matokeo ya matendo
> yako mwenyewe… (uk. 129)

Mwandishi anatumia ishara za sauti ili kumwonyesha msomaji mwanzo wa mabadiliko. Sauti hizi zinachora picha ya mkinzano wa kimawazo kati ya watawala na watawaliwa. Wananchi wanaonekana kuwa na ujasiri mkubwa unaowasaidia katika utetezi wa haki zao.

**2.4.2.5 Taswira ya Joto**

Ni taswira ambazo zimetumiwa kwenye tamthilia hii kuonyesha hali inayosababishia wahusika joto au ukosefu wa utulivu kwa wahusika unaozua wahka na wasiwasi. Wahusika wanaonekana wakiwa na wasiwasi mwingi moyoni na hali hii inasababisha kuwepo kwa joto. Hali hii hutokana na changamoto fulani ambazo zinamkumba mhusika katika kipindi fulani.

Katika tamthilia ya *Kivuli Kinaishi* taswira hii inadhihirika pale mtolewa alijitolea kupambana na uongozi wa Bi. Kirembwe ili awaokoe wananchi kutokana na dhuluma na unyanyasaji. Kwa mfano tunaelezwa:

> Mtolewa: Najiamini kama mchawi yeyote anavyojiamini
> kuchovya mkono wake katika kaango la Juji la
> uwele na kujua kwamba hataungua au kubabua
> mkono wake… (Uk.108)

Mazungumzo haya yanachora taswira ya hali ya joto iliyomkumba mtolewa baada ya uamuzi wake wa kuongoza mapinduzi. Hatua yake iliashiria hatari iliyokuwa mbele yake kwa sababu Bi. Kirembwe alijulikana kama kiongozi dhalimu aliyeangamiza yeyote aliyetishia kumung’oa mamlakani. Udhalimu huu ndio unaolinganishwa na maangamizi yanayosababishwa na moto na hivyo kuibua taswira ya joto.

## 2.5 Tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*

Tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ni tamthilia iliyoandikwa hivi karibuni mwaka wa 2016. Sawa na tamthilia zingine za awali za S.A. Mohamed, tamthilia hii imedhihirisha maendelezo ya matumizi ya taswira kama ilivyodhihirika kwenye tamthilia zake za awali.

### 2.5.1 Muhtasari wa *Mashetani Wamerudi*

Mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ametumia mtindo wa fasihi Andishi na ule wa fasihi Simulizi. Mtindo huu wa uandishi unaifanya tamthilia hii kuwa na nguvu ya kuteka akili za wasomaji wake kutokana na mvuto wake. Wasomaji wanapata ari za kujitafuta kwenye utamaduni wao wa maisha, kisiasa na kiuchumi ili waepuke kumezwa na wimbi la utandawazi unaonea kwa kasi kama moto kwenye chaka kavu. Tunaelezwa:

> Sauti ya mtu: … majumba ya kifahari yanajengwa na mtu mmoja. Majumba ya kiasi cha sabini na tatu.Kisha tazameni kibanda kile kidogo. Kimesimama tisti. Ndani atatoka mtetezi. Atakuja Profesa Hafi- Leo- Wala- Kesho mtetezi. Pole pole ataingia uwanjani- uwanja wa Utandawazi (Uk. 2)

S.A. Mohamed katika tamthilia hii ya *Mashetani Wamerudi* anaonyesha kuwa elimu ya kikoloni imeleta mgawanyiko kwa wananchi na kusababisha uadui wa kitabaka katika jamii. Waliofanikiwa kupata elimu wanaitumia kujinufaisha wao kwa kujitwalia mali, uongozi na nafasi zingine za kujinufaisha. Anaeleza yafuatayo kupitia mhusika Mzee Jumai:

> Mzee Jumai: Aaa, wewe Kitarua kila siku ulikuwa mnara unaong’ara nje na ndani ya madarasa yetu ya kujenga taifa jipya mwanzoni mwa uhuru wa nchi yetu. Hasa ulikuwa mweledi wasomo la historia na somo la maendeleo ambalo tulipenda kulitaja kwa kimombo, Development Studies. Tuliongozwa vyema wakati ule ili kumwelewa shetani. Lakini tulikuwa na hamu ya kukusanya mali na fikra za kwenda mbele. Hilo tulidhani ni jambo la kwenda mbele katika nchi yetu. (Uk. 40)

Vibaraka wa wakoloni mamboleo wanatumia nafasi wanazopata kuwanyonya na kuwakandamiza wanyonge ambao wananyimwa fursa hio kwa kukosa elimu. Elimu ya kikoloni inaonekana kutowasaidia wananchi kwani haiendani na utamaduni na mazingira yao. Wananchi wanalazimishwa kuipokea tu kikasuku bila kutathmini ubora na hasara wanazopitia.Tunaelezwa:

> Mzee Kitarua: Mpaka leo hatuwezi hata kutengeneza sindano! Iko wapi elimu ya matakwa yetu? Iwapi elimu ya falsafa yetu? Kwa nini tunaendelea na mafunzo yanayotoka mbali pasipo kutazama karibu yetu?(Uk. 42)

Tamthilia hii pia imetawaliwa na kundi la watu ambao ni kiwakilishi cha watu waliogundua athari za kimfumo katika nchi za ulimwengu wa tatu. Jazanda kama: Sheta, Jogoo, Mbuyu, mzee Jumai na Kitarua zimetumika kuonyesha jinsi wananchi wanaofahamu athari za kutawalia na mfumo mbovu wa uongozi. Shetani mhusika aliyetumiwa kwenye tamthilia hii kusawiri tabia potovu ya viongozi kutowajibika kwa matendo yao maovu.

Prof naye anawakilisha viongozi waliojitolea kwa hali na mali kutetea na kupigania ukombozi wa nchi na wananchi wake. Anamkabili Sheta ambaye ana uwezo mkubwa wa kiutawala wa kuwazuia viongozi wa kiafrika kutimiza wajibu wao. Isitoshe anajaribu kuwatoa vijana katika utamaduni wao.Tunaelezwa:

> Prof: …. Kuachia wazi milango ya biashara,
> uchumi na utamaduni ni suala la tembo na
> chozi juu ya mbuyu! Tembo ana nguvu za
> kutoa. Chozi hana chochote cha kutoa
> isipokuwa sauti yake nzuri. Sisi chozi
> tutafika lini tunakotaka kwenda? (Uk. 19)

Ujumbe tunaoupata katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ni kwamba umoja ndio suluhisho la migogoro inayosababishwa na tofauti za viwango vya elimu, ukabila, rangi na ueneo. Mchezo baina ya Prof, Kijana 1,2,3,4 na Msichana unawakilisha harakati za maisha ya kila siku na mwingiliano wa watu katika maisha ya kawaida. Kutokana na hali hii tunaelezwa:

> Prof: Tushikamane mtu kwa mtu. Kundi kwa kundi.
> Mwananchi kwa mwananchi. Nchi kwa nchi.
> Udhaifu umo katika kutawanyika.
> Umoja na mshikamano ni silaha zetu. (Uk. 30)

Mwishoni mwa tamthilia hii Prof anaungwa mkono na wazee ambao walikuwa na mtazamo hasi kuhusu mapinduzi (mzee Jumai na mzee Kitarua) hapo mbeleni. Wote wanashirikiana kuwaelimisha vijana kuhusu haja ya kuikomboa nchi yao dhidi ya Ukabila, Utabaka, uzorotaji wa uchumi, siasa duni nadhuluma za kidini.Tunaelezwa:

> Prof: Ubaya ni kwamba tumegawika kimakabila.
> Pia tumegawika mno kimatabaka, kiuchumi,
> Kisiasa na kidini. Mpaka sasa hatujali sana
> nchi yetu. Tunajali nafsi zetu na familia zetu
> na marafiki zetu na makabila yetu.(uk. 64)

Kwenye kilele cha tamthilia hii mvutano unapanuka zaidi baada ya kifo cha ajabu cha Profesa Hafi-leo-Wala-Kesho. Hali hii inazua tanzia pamoja na uzinduzi wa vita vya ukombozi.

### 2.5.2 Taswira katika *Mashetani Wamerudi*

Taswira katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* zimetumiwa kama picha ya kitu kinachofahamika katika jamii inayohusika ambacho ni alama ya kitu kingine kinachoeleweka na wanajamii wengi. Ishara zinazotumika kitaswira huwa na maana mbili. Yaani maana ya moja kwa moja na maana ya kitamathali. Taswira hizi tumeziainisha katika makundi mbalimbali:

#### 2.5.2.1 Taswira za Kiishara

Taswira za kiishara katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* zimetumiwa kuonyesha namna kitu kimoja kimetumiwa kuwakilisha kingine. Taswira hizi zimetumiwa ili kuwasilisha wazo au mawazo kisanaa.

Matumizi ya jina Sheta (Shetani) ni ya kiishara. Jina hili limetumiwa kuwakilisha ukoloni mamboleo ambao upo katika jamii. Baada ya ukoloni mkongwe kumalizika jamii za kiafrika ziliingia katika utawala mpya wa ukoloni mamboleo ambapo anayetawala anakuwa haonekani kama vile ambavyo huwezi kumwona Shetani. Tunaelezwa:

> Sheta: Si unajua kwamba tuna mazingaombwe. Tena
> ni wepesi kwetu kuwapa watu ugonjwa wa
> kizunguzungu. Ndio maana mmetupa jina la
> Kizunguzungu? (uk. 20)

Neno mbuyu nalo limetumika kuwakilisha eneo ambalo matabaka haya mawili hayawezi kukutana. Hapa linaashiria kwamba tabaka tawaliwa haliwezi kulikamata tabaka tawala. Yeyote anayehusishwa na mbuyu ni mfuasi wa serikali.Mwenye mawazo hasi hatakiwi kuukaribia mbuyu. Hapa ndipo mtunzi anafafanua kwa kusema:

> Askarikanzu: Si kosa kukaa kwenye shina la mbuyu na kukusanyika. Kosa ni kwamba tumewasikia mkipanga mipango ya kuharibu mwenendo wa serikali. (uk. 67)

Jina mbuyu vilevile limetumika kama taswira ya mandhari ya nchi za kiafrika. Hali hii inatokana na haja ya wakoloni kuupigania ‘mbuyu’ na kutaka kujificha humo kutokana na uzao wa matunda yake. Tunaelezwa:

> Prof: Shina la mbuyu, shina la mbuyu walibadilisha jiti kubwa lenye virutubishi. Wakalifanya tanda lao la kulalia na kisha pahala pa kurukia katika maendeleo yao. (Uk. 7)

Sherehe zinazoitwa za *Waltz* zimetumiwa kiishara. Hizi ni sherehe ambapo watu hucheza, kunywa na kufurahi. *Waltz* ni densi ya kigeni inayoashiria utamaduni tofauti na wa Kiafrika. Kuwachezea watu *Waltz* ni kuwaadhiri na kuwafanya wakengeuke. Tunaelezwa:

> Prof: Walewale waliotuchezesha mchezo wa maneno na densi ya Waltz huku akijidai wangeondoka kwenda kwao. Kumbe wangerudi na sisi tumewaita na kudhani ni wa kweli? (Uk. 7)

Togwa ni neno lingine lililotumika kitaswira kuashiria utamaduni wa kiafrika. Hiki ni kinywaji kisicholewesha ambacho hutengenezwa kwa mimea ya kiasili kama vile unga wa mtama. Mwanamapinduzi Profesa anasifia utamaduni wanchi yake kuliko utamaduni wa nchi za kigeni ambao unawakilishwa na kinywaji Coca-cola. Tunaelezwa:

> Prof: Aaaa, togwa tamu hii. Tamu tokea kinywani mpaka damuni. Coca Cola itawezaje kutia fora mbele ya togwa? Basi tu – abrogation, yaani vidonge vya dawa ndani ya sheria ya kufuta na

> kukanusha katika kutuziba vichwa vyetu na kutuchezesha ngoma kwenye TV, ili kibaya kiwe chetu daima na kizuri kiwe chao daima. Kibaya chao kiwe kizuri chetu! Coca Cola si kwa siha wala si kwa ladha yoyote ikilinganishwa na togwa…( uk. 7-8)

Bali na kujulikana kama shetani mwandishi anampa jina jingine la mkoloni wa nchi za Afrika. Kulingana naye Jogoo anaweza kuruka, kukimbia na kujificha bila hata kuonekana. Anaweza kuleta madhara makubwa kwa watu bila hata kujulikana. Sababu hii ndio iliyomfanya Profesa kudai kwamba alimkojolea na kumtolea mashuzi kijana aliyekuwa akimfukuza na kumfanya apatwe na kisunzi. Hii ni ishara ya vita vya viongozi na wananchi wenyewe wanapoandamana wakidai kile wanachokiita haki yao. Humwagiwa maji yanayowasha (kukojolewa) pamoja na kutupiwa vitoa machozi (mashuzi) kila mara wanapoandama. Tunaelezwa:

> Kijana 1: Si mizinga ni mashuzi profesa.
> Profesa: Ha! Ha! Ha! Mizinga ni nini na mashuzi ni nini? Si hayohayo maji ya futi na nyayo? Ukiuliza kuwa hiyo ni mizinga wao wanasema ni mashuzi. Wanakataa mashetani kwa kuwaangamiza watu, huku wanasema hakuna aliyeumia. Aaaa! Ni mashuzi tu hayo…Usimfukuze wala usimkamate. Usiwe karibu naye. Ni hatari kuwa naye karibu. Milele daima utaharibika akili. Uliona alikojoa? (uk 12,14)

S.A. Mohamed ametumia ishara ya remote control kama taswira ya kuonyesha utawala mpya unaotumiwa wa wakoloni mamboleo wa kuwanyanyasa na kuwapokonya wananchi rasilimali zao. Wanasimamia na kukamata mikononi mwao kila sekta ya nchi kwa kutumia kile wanakiita *'remote control'*. Tunaelezwa:

> Sheta: Hapana nguvu yoyote ya kutudhibiti, maana sisi tuko nchini mwetu tunabonyeza remote control. Kwani mmesahau kwamba utandawazi ndio remote control zaidi kuliko ukoloni mamboleo? (Uk. 61)

Katika kuhimiza utangamano na umoja wa wananchi, mwandishi anatumia taswira ya kinyesi cha mbuzi na muungano wa sangara (Wadudu wanaotembea pamoja kila wakati). Kulingana naye, wananchi hawapaswi kamwe kuwa kama kinyesi cha mbuzi

kinachotawanyika. Badala yake anahimiza ushikamano na umoja wakati wanatetea haki zao kama wafanyavyo sangara. Anasema:

> Kijana 1:….kwa wakati ule ulikuwa msemo wa kungojeana tu, huyu aende huku na yule aendelee kule. Katika karne hii hatutaki tuendelee kuwa kinyesi cha mbuzi Kinachotawanyika.Tunataka tuwe sangara kwenye mlolongo wa pamoja. Kama hatutashikana mikono na kwenda upande mmoja, basi sote tutaanguka chini na kuramba mchanga! (Uk. 62)

Neno samaki katika tamthilia limetumika kitaswira. Mwandishi analinganisha Mwafrika na samaki ambaye yuko kwenye hatari ya kuvuliwa na mvuvi wakati wowote. Hapa mvuvi akiashiria mkoloni mwenye nia ya kudhibiti kila kitu kwa hila na njama za kinafiki. Kuna taswira ya utawala wa kidikteta ambapo kufaulu kwa mwafrika kunategemea ruhusa ya mkoloni mwenye uwezo wa kuweka kila kitu mikononi mwake. Unafiki wake wa kujifanya mwema kwa Mwafrika unamwezesha kuafikia azma yake. Tunaelezwa:

> Sheta: Mnasahau kwamba sisi hatufi na uwezo wetu wa kutawala hauporomoki.Wema wetu ndio ndoana ya kuvua samaki. Ubaya wetu hautambuliki.Tunajenga na kubomoa dunia. Tunatukuza na kudhalilisha wajinga wanaosinzia na kulala. Kama nilivyo mwambia binadamu, sisi ni nguvu na nguvu ni sisi. Sisi ni uwezo na uwezo ni sisi (uk.71)

### 2.5.2.2 Taswira za Maono

Mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* amekuza taswira hizi zinazoleta hisia za kuona kwa macho ya kiakili. Taswira hizi hutoa picha inayoonekana wazi wakati msomaji anapitia kazi fulani. Picha hizi ndizo zinazomfanya msomaji alinganishe matukio yanayochorwa akilini na matukio anayoyaona kwenye maisha yake.

Mwandishi anachora picha ya vijana walioketi kwenye mduara karibu na shina la mbuyu. Tunaelezwa:

> Prof: Vijana sasa tuketi chini kwa mduara karibu na shina la mbuyu…duara ni dunia…duara linafinya. Linafumba. Linalinda. Linafanya tutazamane. Kisha tushirikiane.(uk. 30)

Kulingana na profesa, kiongozi wa vijana, duara ni kiwakilishi cha dunia. Kwa hivyo, mkao huu uliashiria kuwa vijana wana uwezo wa kutetea na kumiliki kilicho chao. Duara pia ilionekana kama kigezo mojawapo cha kukuza ushirikianao na utangamano unaoleta ushindi mwishoni mwa harakati zozote. Kwa hivyo, msomaji atapata picha kamili ya kuwa na ushirikianao na watu ikiwa ana haja ya kufaulu kwa kila jambo.

Kulingana na mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* inaonekana wazi kwamba matatizo ndio wimbo unaotawala nchi nyingi za Afrika. Kila mwananchi anakumbwa na matatizo ya aina yake. Watu wanaonekana kujawa na ubinafsi ndani ya mioyo na kutokota akili vichwani (uk 34). Mwandishi anatumia wahusika vijana ili kuchorea msomaji taswira anayoweza kuiona wazi katika jamii yake. Anasema;

> Kijana I: Karibu kumaliza digrii yangu ya uzamili nimekoseshwa malipoya chuo, kwa sababu eti mimi ni mchochezi. Sasa nimo kutafuta kazi, lakini kila pahala naambiwa sina shahada ya kutosha…
> kijana II: Mimi nilimaliza shule ya upili kwa mafanikio mazuri, lakini sikuweza kuendelea na masomo kwani wazazi wangu walikufa ghafla pamoja. Nikaanza kazi ya kuchimba mgodi wa almasi. Jambo nililolichukia ni kupekuliwa mpaka kwenye viungo vya siri kwa kufikiriwa kwamba tunaiba almasi.
> Nilikuwa mgumu kukubali kupekuliwa. Siku moja walinikamata na kunipiga vibaya kwa kiasi cha kunifanya mlemavu. Sababu ikiwa nilikataa kupekuliwa. Nilienda mahakamani angalau nilipwe fidia, lakini wapi!Miaka minne kesi haikwisha. Hatimaye niliambulia patupu.
> Kijana III: Mimi pia nilimaliza shule, shule ya upili. Sikufanya Vizuri kwa sababu babangu na mamangu waliachana. Nilibaki kuingia kwenye vikundi vya muziki visisyokuwa na mapato yoyote. Zaidi ilikuwa burudani tu.
> Kijana IV: Mimi kazi yangu ni kuuza karanga barabarani. Aaa, wako wengi barabarani wanauza hiki na kile bila fanaka yoyote. (Uk.36-38)

Mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ametumia taswira hii ya maono kwa ustadi wa aina yake. Bila shaka ana nia ya kumchorea msomaji picha halisi ya matatizo yanayowakumba vijana ili kumtia moyo msomaji. Wakati huo huo, mwandishi anaelekeza njia zinazoweza kutumiwa ili kukabiliana na changamoto kama hizi. Vijana wanaonekana wakilalamika kila siku hasa kwenye mitandao ya jamii kama vile *Facebook*, *Twitter* na *whatsApp* kutokana na mateso wanayopitia (uk. 34*).* Hata hivyo, mwandishi anawatafutia njia badala ya kuendeleza maisha yao. Hii

ni picha halisi inayoweza kuundika akilini mwa msomaji kwani changamoto hizi zinawakumba vijana katika jamii ya leo.

Rasilimali za taifa zinaonekana kuachiwa watu wachache. Wakubwa tu na sio wale wadogo. Wanaojua na kuelewa kutokana na elimu wanayopata kupitia usomaji wa vitabu na wala sio wasiojua chochote. Demokrasia ya taifa inayokuzwa kwa kupiga kura tu na wala sio ushirikiano wa ngazi za juu na za chini. Watu wote hawana haki ya kushiriki katika midomo ya taifa. Demokrasia hapa inakuja kutoka kwa watu wachache wanaotumia nguvu na wala sio wengi kama inavyotakiwa (uk. 34-35).

Nchi nyingi za bara la Afrika zinayumbishwa na janga la ufisadi. Watu wachache wanaipakata na kuhifurahia nchi kwa sababu inawafaa kwa maslahi yao. Wale wengi wameachwa nyuma kimaendeleo kwa ukosefu wa mapato. Pande zote hizi mbili zinataja neno la ‘ufisadi’, lakini hakuna hata mmoja anayesema wazi ama kuchukua hatua kali (uk. 35).

Utandawazi umewapotosha vijana wengi mno. Umezizika mila na tamaduni nzuri za nchi nyingi za Afrika. Inaonekana watoto hawaheshimu mipaka baina yao na wazazi wao kuhusu maswala ya ngono. Hawaheshimu miiko ambayo inastahili kudhibiti uhusiano wao na wazazi wao. Kila mtu anaelekea kwenye wigo wa kupotosha. Hili linatokana na kupeperushwa kwa utamaduni mpya na vyombo vya mawasiliano ya kiteknolojia ya kisasa kwa jina la utandawazi (uk. 36).

#### 2.5.2.3 Taswira za Masikizi

Hizi ni taswira ambazo zinatokana na hisia fulani za sauti. Taswira hizi zinapotokea huwa na athari zinazotokana na sauti yenyewe. Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* mwandishi ametumia mfano huu wa taswira kwa njia ya kipekee. Kwa mfano, kundi la watu likiongozwa na profesa walipokuwa wameketi wakiangazia mustakabali wa demokrasia ya nchi yao waligutushwa na sauti za mibweko ya mbwa (uk. 60). Katika jamii nyingi za Afrika, mbwa wanapobweka huwa wanaashiria hali ya hatari inayowakabili watu. Kwa hivyo, mibweko hii ya mbwa ilikuwa taswira ya hali fulani ya hatari iliyowakabili wanaharakati hawa wa mapinduzi.

Msimulizi anatumia sauti yakuwika kwa Jogoo kama taswira ya kuonyesha nguvu na utawala wa mkoloni. Namna jogoo anapohangaika kabla ya kukokoreka na kutoa mashuzi ni ishara ya kuweka takribani kila kitu chini ya utawala wake (uk. 10). Sauti

hii anayekosa kuielewa inaweza mponza kwani kuielewa si rahisi. Kulingana na Profesa, sauti hii inaposikika iliashiria kuwa kila kitu kipo chini ya utawala wa wageni na hivyo kutaka chochote ni sharti unyenyekee au upigane ambapo ilikuwa vigumu kushinda vita vyenyewe. Shetani ana uwezo wa kuumiza bila hata kutumia nguvu zake. Kwa mfano akipaparika tu na kutoa mashuzi huleta athari hasi kwa walio karibu (uk.12)

#### 2.5.2.4 Taswira za Mguso

S.A Mohamed ametumia taswira za mguso katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ili kuchora picha ya hisia za kuguswa au kushikwa. Anamwonesha msomaji namna matokeo ya kuguswa yanavyoweza kuwa na athari mbalimbali haswa athari hasi. Anaeleza:

> Kijana I: Mimi ndiye niliyewaambia. Siogopi tena.
> Wakati umefika vijana. Nyuma ya kibanda
> Sheta alijigeuza kuku au bata mzinga,
> akanifukuza. Mimi sikuogopa …Tukafukuzana.
> Mara ushuzi. Kisha harufu ya shuzi ikaniingia
> puani. Ikatapakaa mwilini. Ikanitia kizunguzungu
> cha kizungu. (Uk. 29)

Mwandishi anachora picha ya athari zinazomkumba mtu anayejaribu kupingana na utawala fulani. Anaonyesha jinsi uwezo wa viongozi ni mkubwa kiasi cha kutekeleza matakwa yao hata kama itawalazimisha kutumia nguvu. Wananchi wa kawaida Wanapogusana na hawa watawala wakati wa ghasia hukumbana na mateso ya kurushiwa maji yanayowasha au gesi ya vitoa machozi ambayo mwandishi anayaita ‘mashuzi’.

### 2.6 Hitimisho

Tamthilia za S.A Mohamed tulizochunguza zimebainisha kwamba kuna matumizi ya mbinu mbalimbali za lugha kama vile: tashbiha, sitiari, tashihisi, takriri, taswira, majazi, ishara, na balagha. Tumegundua kwamba taswira ndiyo mbinu iliyopewa nafasi kubwa na mwandishi. Hii ni kwa sababu mwandishi amehusisha kazi zake hizi na uchoraji wa picha na kumfanya msomaji atafakari zaidi.

Taswira anazotumia mwandishi zinalenga kuwapevua akili wasomaji katika hali yao ya maisha ili wapate nguvu za kuendelea kipigania mabadiliko yatakayowaletea haki na usawa katika jamii. Matumizi haya ya taswira yanaafikiana na mihimili ya

nadharia ya kimitindo ambayo Leech (1969) anadai kwamba fasihi haiwezi kuangaliwa kwa undani bila kuchambua matumizi ya lugha jinsi tulivyofanya kwa kuchunguza matumizi ya taswira katika tamthilia tulizochunguza.

Tumebaini kwamba msanii ameegemea mbinu hii sana kwa sababu ameangazia masuala mazito ambayo aliamua kuyaeleza kwa kutumia taswira. Utafiti huu umedhihirisha taswira kama mbinu bora zaidi ya kuwasilisha masuala mazito kwa njia rahisi.

Malengo ya tamthilia tulizochambua ni kuibua matatizo yanayokabili jamii na tabaka tawala na kisha kuhimiza ukombozi na mapinduzi ili kuleta mabadiliko yanayofaa. Kwa hivyo, matumizi ya taswira ndio mbinu mwafaka ya kuwasilisha maudhui ya sampuli hii. Hii ni kwa sababu msanii alikuwa na nia ya kubainisha harakati za mapinduzi lakini kwa njia ya uficho. Isitoshe, matatizo na uovu unaoendelezwa na tabaka tawala unaangaziwa kwa njia fiche sana. Mwandishi amempatia msomaji wa kazi hizi nafasi ya kutafakari ili kupata dhana aliyoikusudia.

# SURA YA TATU

## DHAMIRA NA ATHARI ZINAZOTOKANA NA MTINDO WA MATUMIZI YA TASWIRA KATIKA *PUNGWA, KIVULI KINAISHI* NA *MASHETANI WAMERUDI*

### 3.1 Utangulizi

Katika surahii tumejadili dhamira na athari zinazotokana na matumizi ya taswira katika tamthilia za *Pungwa*, *Kivuli Kinaishi* na *Mashetani Wamerudi.* Tumeanza kwa kutoa muhtasari wa mandhari ya tamthilia hizi. Pia tumeangalia dhamira za matumizi ya taswira na baadaye tumeangalia athari za taswira.

### 3.2 Mandhari ya *Pungwa, Kivuli Kinaishi* na *Mashetani Wamerudi*

Mwandishi wa tamthilia hizi tunaweza kusema kwamba ametumia aina mbili za mandhari. Kwanza ametumia mandhari halisi na pili ametumia mandhari dhahania. Katika mandhari halisi mwandishi anaangazia matatizo yanayokumba nchi nyingi za bara la Afrika. Mambo kama vile udikteta, hongo, uongozi mbaya, hali ngumu ya maisha, umaskini, ukandamizwaji, ukabila na unyakuzi wa mali ya umma ni matatizo yanayokumba mataifa mengi ya Afrika. Kwa hivyo, tunaweza kusema kwamba analenga mataifa halisi na changamoto mbalimbali zinazoyakumba.

Katika mandhari dhahania, msanii ametumia vizuu  na Mashetani hasa katika *Kivuli Kinaishi* na *Mashetani Wamerudi* ambapo walikuwa wakiishi na kutekeleza majukumu ya uongozi. Kwa hivyo tunaweza kusema kuwa mwandishi S.A Mohamed ametumia mandhari mseto katika tamthilia hizi.

### 3.3 Dhamira na athari za matumizi ya taswira

Sura hii imeshughulikia dhamira na athari za taswira tulizomulika katika tamthilia tatu za S.A Mohamed. Kuchunguza dhamira na athari hizi kutatupatia mwanga wa kubainisha jinsi mwandishi alivyotumia taswira hizi kuwazindua wasomaji dhidi ya utawala wa kimabavu, matumizi mabaya ya mamlaka, dhuluma za wanyonge na unyanyasaji.  S.A Mohamed alitumia aina mbalimbali za taswira na kwa kila aina alikuwa na dhamira fulani za kuibua athari mbalimbali kwa wasomaji wa kazi zake.

### 3.3.1 Taswira ya Shetani

Shetani ni kiumbe na malaika aliyelaaniwa kwa kuasi amri za Mwenyezi Mungu. Ni kiumbe kinachofanya matendo mabaya. Jina Shetani kulingana na muktadha huu linaashiria viongozi dhalimu ambao wanawakandamiza wanyonge katika jamii yenye utabaka.

Taswira ya shetani inaashiria viongozi wa kikoloni. Hali ya shetani kumtupia kijana mzinga na kumkojolea ni ishara ya dhuluma na unyanyasaji (*Mashetani Wamerudi* uk.11-12).

Mashetani pia yalidaiwa kumwingia Bwana kichwani na kusababishia Bibiye dhiki kubwa ya kumshughulikia asijue la kufanya. Kila mara alifikiria kwamba kuna njama ya kumnyang'anya mamlaka. Tunaelezwa:

> Bwana: …wewe kichwa ndio chanzo cha yote hayo.
> Kichwa kiti cha shetani na ombe ni kiti changu
> mimi. Wamehozi na kulowea mashetani
> kichwani humu. Wamekiteka kichwaChangu.
> Mawazo yangu yanapeperuka huku na huko,
> hayana makini, hayatulizani, hayatengamani…
> (uk. 40)

Kitendo cha kumtupia kijana mashuzi na mizinga ni kitendo kinachodhibitisha dhuluma na unyanyasaji aliofanyiwa. Hali ya Bwana kutopata utulivu inatokana na wasiwasi kwamba anaweza kunyang'anywa uongozi. Kutokana na tamaa hii ya uongozi, anadaiwa kuwaua wote walioonyesha nia ya kuupinga utawala wake. Tunaelezwa:

> Bwana: Nambie basi, miaka kumi na nane nyuma,
> lilitokea tukio gani…?
> Bibiye: Ulimdidimiza hasimu yako, akadidimia dididi!
> Bwana: Kweli, na baada ya miaka mitano?
> Bibiye: Ulimsagasaga adui yako mkubwa, akasagika
> sagasaga kama unga. ( Uk. 40)

Taswira nzima ya shetani inapelekea msomaji kukumbwa na hofu na huzuni tele. Ni taswira inayotoa picha ya kuchukiza. Pia inaibua ujuzi wa msomaji kuhusu mbinu zinazotumiwa na viongozi kuwadhulumu watawaliwa. Isitoshe suitafahamu kati ya tabaka tawala na tabaka tawaliwa inaangaziwa.

Tunaambiwa hata mashetani huwa na nia mbaya kila wakati kwa watawaliwa. Kwa mfano katika *Mashetani Wamerudi*, mwandishi anasema:

> Sheta: Sisi unajua kwamba tuna mazingaombwe.
> Tena ni wepesikwetu kuwapa watu ugonjwa
> wa kizunguzungu. Ndio maana mmetupa jina
> la kizunguzungu? (Uk.20)

Anayeambiwa maneno haya na Shetani ni Profesa ambaye ametoka katika tabaka la walalahoi. Maelezo haya yanatupatia kiumbe ambaye ana uwezo mkubwa wa kuamrisha katika utawala wake. Ana uwezo wa kufanya atakavyo na kudhibiti takribani kila kitu.

Katika tamthilia ya *Pungwa*, mwandishi anatumia taswira ya kuonekana kudhihirisha jinsi uwezo wa Shetani ni wa kupindukia na unaweza kusababisha mauti. Bwana aliyepagawa anasema kwamba alimzika mpinzani wake kwenye kaburi la kina kirefu kisicho mwisho. Haya yote anayaweka siri (uk.41).

Taswira nzima ya shetani ni ishara ya mitafaruko ya kitabaka na uongozi kati ya watawala na watawaliwa. Uongozi hapa umetumiwa kama silaha ya kudumisha udhalimu katika jamii. Taswira ya shetani inayotumiwa na S.A Mohamed inalenga kumzindua msomaji dhidi ya unyanyasaji unaoendelezwa na viongozi kwa sababu ya tamaa ya uongozi. Mfumo kama huu wa uongozi hautambui haki za binadanu.

Lengo la S.A Mohamed la kutumia taswira ya shetani ni kuwazindua wasomaji wa tamthilia zake ili wapevuke kimawazo na kuwatolea mwanga wa hali halisi ya dhuluma wanazopitia watawaliwa mikononi mwa viongozi wao. Lengo lake kuu la kutumia taswira ya shetani ni kuleta dhana ya udikteta au ukandamizwaji kwa wananchi wa kawaida.

### 3.3.2 Taswira ya kuzunguka Mbuyu

Mbuyu ilikuwa eneo ambalo watu wa hadhi ya chini hawakuruhusiwa kukaribia. Katika muktadha huu, mbuyu unaashiria nguvu na mamlaka ya utawala wa ukoloni. Hata hivyo baada ya uzinduzi vijana walikongamana na kufanya duara karibu na shina la mbuyu ili kuonyesha umoja wao na nia yao ya kutetea haki zao kama nchi. Tunaelezwa:

> Msichana: Sijachelewa kuwa na wenzangu. Nimefika duarani.
> Nimefika kwenye maskani ya Utetezi. Wapi pengine
> pa kushtakia kama si hapa? Ukweli uko wapi?

> Tunaona uongo unaoning'inizwa hewani? Hakuna haja ya kukata kauli. Tuseme tu. Hakuna haja ya kukimya. Hakuna haja ya kufa wakati tuko hai. Kwa nini haturudi kwenye mwanzo uliowafukuza mashetani. Nguvu za umma kila siku zinafaulu…(uk.32)

Maelezo haya ya mwandishi yanaibua taswira ya muungano wa wanamapinduzi walio na uwezo mkubwa wa kutetea na kulinda rasilimali za nchi yao. S.A Mohamed analenga kuwafahamisha kwamba inawezekana kiongozi akang'atuliwa mamlakani na wananchi walioungana iwapo hatatekeleza majukumu yake. Anawazindua wasomaji kwamba mageuzi yanaweza kufaulishwa na umoja na ushirikiano.

Mwandishi anaendeleza taswira hii ya muungano katika tamthilia yake ya *Kivuli Kinaishi*. Hapa Bi Kirembwe alikuwa amezoea kuwanyanyasa wanaginingi katika nchi yao wenyewe. Hata hivyo, baada ya kuzinduliwa na Mtolewa, wananchi walipata kufahamu haki zao na namna ya kuzitetea. Waliungana na kukata kauli ya kumng'oa Bi. Kirembwe mamlakani. Wote kwa pamoja walimwendea. Mwandishi anasema:

> Sauti nyingi: Bi. Kirembwe…leo yamekwisha…kama yalivyoanza. Leo hakuna kizuizi…leo ndio ile Siku yetu na yako…leo ndio leo…tunakuja ndani, hakuna uchawi, hakuna ulinzi (Uk. 127)

Nukuu hii inadhihirisha juhudi za wananchi za kujikomboa kutokana na dhuluma zinazotokana na viongozi wao.

### 3.3.3 Taswira ya Maandamano na Mauti

Taswira ya kuuawa ni taswira nyingine inayoleta hisia za woga na ari ya kutaka kubadilisha mfumo unaopendelea mauaji. Hii ni taswira inayoleta nguvu kubwa ya kukifanya kitendo kigande akilini. Pia kule kuvamiwa na kundi la watu waliooungana ni njia ya kutisha watawala madikteta. Wanaotawaliwa wakigundua uwezo wao hawatataka kukata tamaa katika harakati zao za kutetea nchi yao au tabaka lao.

Katika tamthilia ya *Pungwa*, kundi la watu lilivamia Bwana na Bibiye kwenye maskani yao ili wakomeshe dhuluma na unyanyasaji dhidi yao. Walikuwa wamevaa magwanda, miguu chini na walikuwa wamechukua zana za kupungia…fimbo…marungu…singa…pembe…majani na makome (uk. 50). Kundi hili la watu lilijitolea kwa kile walichodai kuutibu ugonjwa wa Bwana. Tunaelezwa:

> Simba: Tunajua kwamba wewe ni mgonjwa na
> unahitajia kupungwa na hapana mtu mwingine
> wa kukupunga isipokuwa sisi watu, kundi
> letu, sote!!! Sisi sote si mmoja. Sisi sote,
> wingi wetu, kundi lote, sote!!(uk. 52)

Baada ya kauli ya mmoja wa wanamapinduzi kufaulu (Simba), wote walijitolea kuleta mwamko mpya katika nchi yao. Waliwavamia na kuwang'oa mamlakani viongozi walioendeleza dhuluma na ubinafsi miaka na mikaka. Mapinduzi haya hayakuwa rahisi kuyatekeleza. Bwana alibanwa kichwa hadi akakubali masharti ya kuacha utawala. Walivamiwa na kundi la watu na kuondolewa kutoka kwenye jukwaa ambapo hali yao haikujulikana kutoka hapo (*Pungwa* uk. 55).

Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, umma ulichoshwa na uongozi wa mashetani na marafiki zao. Uliamua kuandamana ili kupigania haki za tabaka lao. Tunaelezwa:

> Umma:Sisi ni wananchi… Hii ni nchi yetu…
> Hatutaki kutawaliwa kwa remotecontrol…
> Rasilimali zetu ziwe mikononi mwa
> wenyeji… Biasharaiwe nipe nikupe.
> Viongozi wetu wawe macho… Viongozi
> wetu wawe na sisi wasiwe na mashetani.
> Vijana wafanyiwe mbinu za kupata kazi…
> utamaduni wetu una mengi
> ya kukubalika…(uk. 74-75)

Wananchi waliandamana wakiongozwa na Profesa. Aliwaelekeza kwa ushauri wa mbinu na njia za kutumia kwenye maandamano yao. Hata hivyo, Umma huu ulikabiliana vilivyo na askari hata baada ya kurushiwa mabomu ya kutoa machozi (uk. 76). Hatimaye maandamano haya yalisababisha kifo cha kiongozi wao (Profesa). Alifariki lakini akaacha kauli ambayo iliwatishia viongozi dhalimu baadaye. Anasema: *Naiwe buriani ya leo au kesho. Lakini ujue nikifa mimi kuna kama mimi ambao daima wataitetea nchi yetu* (uk. 79).

Katika tamthilia ya *Kivuli Kinaishi*, Mtolewa aliongoza wari wengine kwenye harakati za kujikomboa na kuikomboa nchi yake. Aliwaunganisha ili kuwazindua na kuwafanya waelewe zaidi kuhusu haki zao. Aliwaambia:

> Mtolewa:Wacheni woga wenu! Msibabaike! Msishtuke! Msishtuliwe na vicheko hivi—vicheko vingi tu, vimejaa, vimesambaa, vimetuzunguka; hivyo mnavisikia kwa sababu ndio kwanza masikio yenu yazibuke. Bado mtavisikia vicheko vingi, lakini nyinyi vipuuzeni tu—muhimu mtambue kwamba kuanzia sasa nyinyi mko huru kimawazo… (uk. 101)

Baada ya kujitolea kuwaongoza wanamapinduzi, Mtolewa alifarakana na Bi. Kirembwe. Hali hii ilimkasirisha sana Bi. Kirembwe na aliiona kama uasi. Ni hali aliyoiona kama ya kudidimiza Giningi. Hatimaye alitoa amri ya kuuawa kwa Mtolewa (Uk. 114).

Kwa kutumia aina hii ya taswira,S.A. Mohamed alilenga kuwazindua wanaharakati wa mapinduzi ili awape nguvu za kuendeleza mapinduzi. Anawaonyesha njia zinazotumiwa na viongozi kwa lengo la kuwatishia wanaharakati ili wakomeshe vita dhidi ya tabaka tawala. Taswira hii inachochea mwamko mpya. S.A Mohamed alilenga kupendekeza mapinduzi kwa wale wanaonyimwa haki na kunyanyaswa na watu walio mamlakani. Aina hizi za taswira zinaweza kuibua athari za kutaka mageuzi kwenye nafsi ya mtu na ili ndilo lilikuwa lengo lake Mwandishi. Taswira za mguso zilizosababisha mateso ya Mtolewa na Profesa zimetumiwa na S.A Mohamed kuonyesha hali ya dhuluma, ukatili na uhasama unaondelezwa na watawala. Viongozi lengo lao ni kutetea na kulinda haki za watawaliwa lakini viongozi tunaowaona katika tamthilia ya *Pungwa, Kivuli Kinaishi* na *Mashetani Wamerudi* ni dhihirisho la ukiukaji wa haki za binadamu.

S.A Mohamed pia anaibua haja ya kuwa na mapinduzi katika utawala. Mapinduzi haya yanalenga mfumo wa kisiasa, kijamii na kiuchumi kama vile tumeangazia. Sera ya jamii kuhusu nafasi yao katika utawala na sera ya utawala wenyewe inatakiwa kubadilika au kubadilishwa. Huu ndio uliokuwa mwito wa S.A Mohamed alipotumia taswira katika tamthilia zake za *Pungwa*, *Kivuli Kinaishi* na *Mshetani Wamerudi.*

Mateso wanayopitia watu wa tabaka la chini katika tamthilia hizi yanapelekea msomaji kupata hamu ya kutaka kubadilisha hali hii. Hali ngumu waliyopitia wanamapinduzi na mateso ya kila ainahali inayomfanya wasomajiwajawe na hisia tele za uozo katika jamii zao na kushangaa ni vipi binadamu awe adui wa binadamu mwenzake kiasi kile. Kwa hivyo, taswira inayoibuliwa na mwandishi inanuia kudhihirisha jinsi makabwela wanadunishwa na kunyanyaswa na watu wa tabaka la kikabaila. Hii ni taswira yenye uhalisia katika jamii ya mwandishi wa tamthilia hizi. Tunaweza kuhitimisha kwa kauli kuwa S.A Mohamed amefaulu kuonyesha msomaji mfumo wa kitabaka usio na usawa na ambao hukandamiza maskini.

### 3.3.4 Taswira ya Makabwela na Makabaila

S.A Mohamed anatumia taswira hii ili kuonyesha tofauti iliyopo baina ya tabaka la juu na la chini. Taswira hizi zinalenga kuleta mwamko mpya ambao hatima yake ni kuleta mapinduzi yatakayoleta usawa katika jamii. Taswira ya kuonekana ya makazi ya kifahari ya watawala ikilinganishwa na yale ya wachochole inaamsha ari ya wasomaji ya kutaka kuporomosha mfumo wa kiutawala wenye matabaka. Jamii zozote zenye kuendeleza mfumo wa kitabaka haziishi mikwaruzano.

Katika tamthilia za Mohamed za *Pungwa, Kivuli Kinaishi* na *Mashetani Wamerudi*, taswira hizi anazimulika kwa njia wazi. Katika *Pungwa*, mwandishi anasema;

> Bibiye: Mimi naishi katika dhahiri ya mambo.
> Naishi leo, sio kesho wala jana. Naishi
> maisha ya rutuba, chakula na maji kujineemesha.
> Naishi katikaukweli wa jinsi moja kuiangamiza
> jinsi nyingine. Naishi katika uchaguzi wa rafiki
> na adui.Singojei wala sina muhali. Jicho kwa jicho,
> pua kwa pua. Huitetea jinsi yangu kuinakamisha
> jinsi nyingine. (Uk. 7)

Taswira ya Bibiye hapa imejengeka kwenye istiari. Bibiye anaonekana anapata lishe bora kama inavyolinganishwa na rutuba. Kwa kawaida binadamu anayejidai kuishi maisha yenye rutuba husemekana kama ameridhika. Bibiye katika tamthilia ya *Pungwa* amesawiriwa kuwa ameridhika kutokana na maisha anayoishi yasiyojua taabu yoyote. Kuridhika huku kumesababishwa na unyonyaji wa wanyonge.

Jumba la kifahari wanamoishi  Bwana na Bibiye pia linatoa taswira hii. Baada ya wananchi kukata kauli na kuivamia jumba la Bwana na Bibiye, walipata makubwa. Walijifungulia redio na TV. Walionekana kufurahia maisha waliyoyapata humo.

Isitoshe, walikula matunda matamu yaliyokuwa juu ya meza. Wengine walisema hawajawahi kula matunda matamu kiasi kile. Wakashangaa namna watu wawili wanaishi jumba lote hilo (uk. 51).

Katika tamthilia ya *kivuli Kinaishi*, mwandishi ameyachora maisha ya wachochole kama yaliyotengana kama usiku na mchana. Haonyeshi dalili zozote za tabaka la chini kufikia tabaka la juu. Walionavyo wanaendelea kupata zaidi huku wanyonge wakiendelea kuteseka. Wenye mamlaka hawataki kamwe kusikia kwamba uwezo wao unaweza kufikia ukingoni. Wanalinda uongozi wao kama mboni ya jicho. Tunaelezwa:

> Bi Kirembwe: …wakati haubadiliki. Wakati haugeuki ni uleule tu. Jana ni jana na leo ni leo na kesho ni kesho, mtondo na mtondogoo na saa zake na nukta zake ni zilezile…kinachogeuka ni roho za watu kwa tamaa na choyo; watu wanaosahau kwamba kila mtu ana daraja yake. Wengine tumezaliwa tukalie viti, wengine wakalie makumbi; wengine wahukumu na wengine wahukumiwe (Uk.123)

Kwenye tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, mwandishi anaibua hali ya utengano pia. Anachora taswira ya hali halisi ya maisha ya wenye navyo na wasio navyo. Maoni yake yanadhihirisha namna wachache hufurahia matunda ya nchi yao huku halaiki iking’ang’ania nafasi ya kuishi katika nchi yao wenyewe. Tunaelezwa:

> Kijana 3: Tatizo jingine ni la uchafu. Uchafu wa roho zetu zinazotofautisha baina ya makundi ya wachache na wengi. Wachache wanaipakatana kuhifurahia nchi kwa sababu inawafaa kwa mapato na maslahi yao.Wengi wanaitemea mate na kuichukia nchi yetu kwa sababu haiwafai kwa ukosefu wa mapato na maslahi yao… (Uk. 35)

Taswira nzima ya utengano wa walalahoi na walalaheri si geni. Kwa mfano, katika nchi nyingi za Afrika, wakwasi huwa na mitaa yao ya aina yake inayolindwa na walinzi ambao huwaajiri wao au hupewa na serikali. Wao hutangamana na watu kwa nadra sana isipokuwa watu kutoka tabaka lao. Mchochole yeyote yule haruhusiwi hata kuyaona majengo yao kutokana na nyua ndefu zilizoezekwa vigae vya chupa au hata nyaya za stima na wengine hata ulinzi wa Majibwa na askari kwenye malango.

Kutokana na taswira hii ya utabaka, S.A. Mohamed anamchorea msomaji wa tamthilia hizi hali halisi ya maisha katika nchi yake. Taswira hii inayolinganisha nafasi za maisha baina ya makundi mawili ina nguvu kubwa ya kunata kwenye akili ya msomaji na kumpa uwezo wa kuzinduka iliatie juhudi za kuubadilisha mfumo wenye utabaka.

Taswira anazoangazia S.A Mohammed ni halisia na uthabiti wake upo katika kuangazia hali ya mambo katika nchi nyingi za bara la Afrika Kenya ikiwa miongoni mwao. Zinaamsha hisia za msomaji na kumpa ari ya kutaka mabadiliko hata kama itawagharimu kujiingiza katika harakati za mapinduzi ili kupunguza au kumaliza utabaka katika jamii yao.

### 3.3.5 Taswira ya Wanamapinduzi

Taswira ya kuonekana ya harakati za kuanzisha mapinduzi yanayoongozwa na Simba, Mtolewa na Profesa katika tamthilia za *Pungwa, Kivuli Kinaishi* na *Mshetani wamerudi* mtawalia. Kiu ya kutaka kumaliza udhalimu, utabaka na ukosefu wa haki na usawa katika jamii ni dhahiri kwa wasomaji wa tamthilia hizi. Kwa mfano, katika tamthilia ya *Pungwa* tunaelezwa:

> Simba: …tunayekwenda kupambana naye ni kama
> nilivyokwambieni ni mtu mwenye
> shetani wakubwa na wenye nguvu nyingi na
> mazingaombwe makubwa. Wingi wetu
> sisi ndio nguvu zetu kubwa- bila ya
> huo hatutafanikiwa: wingi na mazingaombwe bila
> shaka… na mbinu zetu: tutashinda tu!
> Lakini lazima tufuate yote tuliyoyapanga;
> hakuna woga, hakuna kurudi nyuma,
> lazima tupunge mtu huyu shetani wake
> wote.(Uk. 50)

Picha hii ya wanamapinduzi waliokakata kauli kwa ushujaa na ujasiri kutaka kubadilisha hali yao inachochea mwamko mpya kwa msomaji. Inaashiria mwisho wa makabwela kuvumilia kunyanyaswa huku makabaila wakijivunia kumiliki rasilimali kwa nja za mkato. Wanaharakati wanaonekana wamejitolea mhanga ili angalau wabadilishe hali zao hata kama watalipia gharama kubwa.

Katika tamthilia ya *Kivuli Kinaishi,* wanamapinduzi wako tayari hata kufa ili kuikomboa nchi yao. Tunaelezwa:

> Mtolewa: …najua kuwa nitababuka----nitaangamia pengine: lakini nyama ya mwanadamu inaweza kubabuka, ikaoza… lakini kivuli na roho yake haiwezi ikaoza….(uk.109)

Taswira hii ya kujitolea mhanga kwa wanamapinduzi inawapa wasomaji msukumo wa kutambua kwamba wao wenyewe ndio wenye uwezo wa kuleta mabadiliko katika jamii. Dhuluma wanazopitia zinawekwa bayana na mwandishi katika tamthilia yenyewe ili wagundue kuwa wanateswa na kwamba wamenaswa katika minyororo ya kiuchumi, kijamii, kitabaka, kielimu, kitamaduni na kimawazo na hivyo wanatakiwa kujitahidi ili wajikomboe. Tunaelezwa:

> Kijana 1: …mmetumezesha fikra mbovu za uchumi, utamaduni na mwenendo wa kijamii ndani ya mfumo wa elimu. Mpaka sasa tumedhoofika kwa kumeza fikra zenu.( uk. 49)

Ukombozi kulingana na S.A Mohamed huleta wasiwasi mwingi kwa viongozi waliozoea kuongoza kwa kutumia nguvu. Huwa hawatulii hasa wakigundua harakati zozote za mageuzi zikipangwa. Tunaelezwa:

> Bwana:… hao wameshafika karibu. Wapo labda wewe huwaoni wingi wao ndio unaonitisha….hao, kundi zima linatoboa ukuta. Wingi wa watu kumbe huweza kutoboa ukuta wa kangriti na chuma!... (uk. 42)

Maneno haya yanaashiria kuwa viongozi dhalimu hupatwa na woga haswa wanapotambua kuwa kuna harakati za kuwaondoa mamlakani. Hata wakati mwingine viongozi wanaota wakikabiliana na nyoka. Tunaelezwa kwa mfano:

> Bwana: Nyoka huyo...naapite
> yuko mlango wanje, naapite
> yuko mlango wa ukumbini, naapite
> yuko mlango huo hapo wa chumbani,
> naapite nyoka huyo hapo…. (Uk.44)

Hapa nyoka si mnyama wa kawaida. Ni nyoka hatari sana na sumu yake inaweza kuua mara moja. Mapinduzi yanaweza tokea mara moja na hili ndilo S.A Mohamed alikusudia kuwamulikia wasomaji. Taswira ya nyoka inaweza kumtia mtu woga sana.

Iwapo viongozi hawa wanaweza kuogopa mapinduzi kama vile wanaogopa nyoka, basi huenda wakalazimika kukokemesha dhuluma dhidi ya watawaliwa.

### 3.3.6 Taswira ya Mwanamke

Mwanamke katika kazi nyingi za fasihi huchorwa kama kiumbe dhaifu chenye nafasi ya chini na kama chombo cha kumfurahisha mwanamume (Kiango, 1992). Katika tamthilia hizi tatu tulizochunguza, mwandishi amechora mwanamke kama shujaa, kiongozi dikteta na si kiumbe duni tena. Mwanamke katika *Mashetani Wamerudi* amechorwa kama mwanamapinduzi. Yumo msitari wa mbele kupigania haki na mabadiliko katika jamii. Tunaelezwa:

> Msichana: ...nimefika kwenye maskani ya utetezi.
> Wapi pengine pakushtakia kama si hapa?
> Ukweli uko wapi? Tunauona uongo
> unaoning'inizwa hewani? Hakuna haja ya
> kukata kauli. Tuseme tu. Hakuna haja ya
> kukimya. Hakuna sababu ya kufa wakati
> tuko hai. Kwa nini haturudi kwenye
> mwanzo uliowafukuza mashetani. Nguvu za
> umma kila siku zinafaulu ( Uk.32)

Kwenye *Kivuli Kinaishi*, mwanamke amechorwa akiwa na sura mbili. Yeye ni mtawala wa kidikteta na pia yeye ni mwanamapinduzi. Bi. Kizee anaonekana wazi akichukia matendo maovu ya Bi. Kirembwe na viongozi wengine wa Giningi. Anasema;

> Bi. Kizee: …Tumeshindwa kufanya cha maana
> kwa sababu roho zetu zimejaa magonjwa
> ya miaka ya ubinafsi …tama … choyo …
> uadui na uhasama … ajabu… (Uk. 78)

Chuki ya Bi. Kizee inatokana na namna viongozi wanavyowadhulumu wananchi wa kawaida. Bi. Kizee yupo msitari wa mbele katika kutetea haki na usawa kwa wote. Anadai kwamba uchukivu huja kwa njia ya kuona yanayochusha kama vile unafiki, maonevu na kuona mwanadamu akifuata mambo kama zuzu lililoletewa akili…(uk. 78). Kwa hivyo, mwanamke huyu anapigania mageuzi bila woga na amejitolea kuwapa vijana wosia ili wasikubali kutumiwa na viongozi kwa ajili ya manufaa yao.

### 3.3.7 Taswira ya Askari

Taswira ya askari imetumiwa na S.A Mohamed katika tamthilia tatu zake. Ananuia kuwapa wasomaji mtazamo mpya kuhusu viongozi na walinzi wao. Askari

wanaonekana kutumia uwezo wao na kuwanyanyasa raia. Raia wananyimwa haki zao na kukandamizwa kupitia uongo. Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi,* askarikanzu wanatumiwa na viongozi kuwanyanyasa wananchi haswa wanaojumuika kupanga mikakati ya kuleta mapinduzi. Wanawatahadharisha wananchi dhidi ya kupanga mipango kinyume na serikali. Tunaelezwa:

> Askarikanzu1: … mbona mmekusanyika? . .
> si kosa kukusanyika. Kosa
> ni kwamba tumewasikia
> mkipanga mipango ya
> kuharibu mwenendo wa
> serikali… basi mtaona
> kilicho mfanya sangara kuchomwa
> moto. (Uk. 66, 67)

Viongozi wengi hutumia askari ili kuwavuruga wale wanaoonekana kupinga sera zao. Wanafanya hivyo kwa kudai kwamba wanamapinduzi hawa wanataka kutumia vijana ili waende kinyume cha utawala. Tunaelezwa:

> Askarikanzu 2: Mnawavuta vijana ili mwende kinyume cha nchi.
> Mzee Jumai: Hilo pia si kosa. Kwani nchini mwetu hakuna
> kauli moja. Nyinyi mmetumwa ili kuvuta vijana
> kwenda kinyume cha nchi.(Uk.67)

Katika tamthilia ya *Kivuli Kinaishi*, walinzi walitumiwa kuwanyanyasa wananchi. Mwananchi yeyote aliyekosa kutoa hongo alizuiwa kuingia kwenye Giningi. Tunaelezwa:

> Mtolewa:….nyinyi mnaojua yote. . . mpasao kukunjuliwa
> mikono mirefu hatukuja hivi hivi sisi, hatukuja
> na domo kaya, hatukusahau kanuni na maisha
> ya siku hizi. A-a, hapana aliyetaja hongo hapa,
> tunachosema ni kwamba mtaka uzuri dhurika,
> mtaka kupanda-juu, kila kipandio kina
> mbinu zake… (Uk.28, 29)

Kupitia kwa taswira hii, S.A Mohamed alilenga kuwazindua wasomaji wa tamthilia hizi kwamba katika kitengo cha utawala, askari wanaopaswa kulinda wananchi huwa na siri zao za kuwabagua kulingana na vile wana uwezo wa kutoa kiasi fulani cha hongo. Askari hawaongozwi na maadili ya kazi ila ubinafsi na tamaa. Ukitoa 'chai' kwao bila shaka utakuwa na bahati ya kufika popote utakapo na zaidi ya yote kutambua siri kali za serikali. Tunaambiwa kwamba baada ya Mtolewa kupeana

bahasha, alikubaliwa kuingia Giningi kisha akakaribishwa kwa heshima kuu na bawabu. Tunaelezwa:

> Babu II: . . .Unasubiriwa kwa hamu ndani…
> Ingia, na ukisha ingia keti juu
> usikubali kuporomoka chini.
> Chini kuna udhia--- pita mtolewa
> pita Giningi (Uk.30)

S.A Mohamed alilenga kuwazindua wasomaji kuhusu ufisadi unaoendelezwa na walinda usalama. Katika taswira hii unafiki wa askari unafichuliwa. Mtazamo huu mpya wa msomaji unalenga kumwongezea hisia za ukakamavu ili ajisatiti kupigania mabadiliko katika jamii yake.

### 3.4 Hitimisho

Sura hii imebainisha kwamba S.A Mohamed ametumia mbinu ya taswira kwa jinsi ya kipekee akiwa na malengo maalumu. Utafiti huu umebainisha jinsi anavyozitumia taswira hizi ili kuzindua wasomaji wake kuhusu uhalisia wa mambo katika maisha yao. Pia, S.A Mohamed ametumia taswira hizi kama silaha ya kuamsha hisia za wasomaji wa tamthilia hizi ili wabainikiwe na hali halisi ya mambo wanayopitia. Taswira alizotumia zina msukumo mwingi na huweza kuisugua akili ya msomaji na kumwangazia hatua mwafaka ya kuanzisha harakati za mapinduzi yatakayowaondoa madikteta kwenye mamlaka.

Kwa upande mwingine, taswira anazozikuza zinalenga kufungua wasomaji akili na kuleta hamu ya mabadiliko ya kujenga jamii mpya. Isitoshe, ameangazia kufaulu kwa mapinduzi yanayoletwa na watu wengi katika jamii. Pia, matokeo hasi ya athari za utabaka katika jamii yamemulikwa.

Kwa ujumla, taswira anazozitumia zinanuia kuwazindua wasomaji kuhusu uyakinifu wa maisha yao ili wapate motisha ya kuanzisha harakati za ukombozi na kuleta mabadiliko katika jamii zao. Taswira hizi zinaonekana kufaulu kupitisha ujumbe kwa njia iliyo bora zaidi kwa sababu mwandishi hakuzitumia kwa ulegevu bali kwa ukwasi na ustadi mkubwa katika kuelezea yale anayohisi (Coombes, 1953).

S.A Mohamed amefanikiwa kutumia lugha kwa namna ifaayo kupitia matumizi ya taswira. Uzoefu wake wa kutumia taswira unadhirishwa kikamilifu na mihimili ya nadharia ya umitindo tuliyotumia kwenye utafiti huu. Kulingana na Leech (1969), fasihi si fasihi bila kuzingatia matumizi ya lugha.

# SURA YA NNE
# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 4.1 Utangulizi

Lengo la utafiti huu lilikuwa kubainisha aina za taswira katika tamthilia za *Pungwa* (1988), *Kivuli Kinaishi* (1990) na *Mashetani Wamerudi* (2016). Lengo letu pia lilikuwa kuonyesha dhamira ya matumizi ya taswira pamoja na athari zake kwa hadhira lengwa. Kutokana na utafiti huu, tamthilia hizi zimeonekana kuinua hadhi ya taswira kama mbinu bora ya lugha ya kuwasilisha ujumbe mzito.

Tasnifu hii imechunguza matumizi ya taswira kwa kina katika tamthilia tulizoteua na kudhihirisha ufaafu wake katika uwasilishaji wa maudhui mazito kwa njia rahisi. Kwa kuchunguza taswira mbalimbali, tumeeleza namna masuala yanayoleta utata yanaweza kuwasilishwa kwa hadhira bila ya kuzua mfarakano wowote.

Tamthilia tulizoshughulikia zimedhihirisha matumizi ya asilimia kubwa ya taswira kuliko mbinu nyingine ya lugha. Taswira hizi zimetumiwa na mwandishi hasa kuibua na kuendeleza harakati za kimapinduzi kwa njia isiyo ya kawaida.

## 4.2 Muhtasari wa matokeo ya utafiti

Kutokana na utafiti huu, tumebaini kwamba taswira ni mbinu iliyotumiwa na mwandishi ili kuwazindua wasomaji waweze kuona uhalisia wa maisha katika jamii zao. Tumebaini kwamba mwandishi ametumia taswira mbalimbali kama za shetani, mbuyu, askari, wanamapinduzi pamoja na taswira ya makabwela na makabaila ili kumfungua macho msomaji kuhusu athari zinazotokana na uongozi wa kitabaka. Mwandishi huyu tunaweza kusema kwamba alilenga kuibua haja ya mapinduzi katika sekta mbalimbali kama; mfumo wa kisiasa, kielimu, kiuchumi na kijamii. Kupitia mapinduzi haya, mwandishi anampa msomaji ndoto hai ya kuleta haki na usawa wa ugawaji wa raslimali za nchi, uongozi, elimu miongoni mwa maswala mengine.

Taswira ya shetani inaonyesha udikteta unaotokana na mfumo wa uongozi usiozingatia usawa katika jamii. Tabia za shetani za kuwasumbua watu na kudai kutawala kila pahali bila hata kuonekana zinawazindua wasomaji kuhusu umuhimu wa uhuru wao wa kujitawala wao wenyewe. Imedhihirika kwamba walioambukizwa utawala wa kikoloni ni dhalimu zaidi kuliko wakoloni wenyewe. Katika tamthilia ya

*Pungwa*, Bwana alidaiwa kuwa na Shetani wawili. Yule wa kitamaduni na yule wa kigeni. Lakini huyu wa kigeni alidaiwa kuwa na uwezo mkubwa wa kumiliki kila kitu.

Taswira ya unga wa ndere uliotumiwa na Bi. Kirembwe inalenga kufichua unafiki wa viongozi kwamba wakati mwingine viongozi hutumia uongo ili wadumu mamlakani. Wanaokiuka amri za serikali zao huishia kuondolewa njiani kwa kuangamizwa. Bwana katika *Pungwa* alijivunia kuwaua watetezi kadhaa waliokuwa na kiu ya kuleta haki kwa wanyonge. Vivyo hivyo, profesa katika *Mashetani Wamerudi* aliuawa kutokana na juhudi zake za kupigania mapinduzi. Kulingana na S.A Mohamed, viongozi dhalimu wanapaswa kuondolewa ili kuunda serikali inayozingatia haki.

Taswira ya jogoo, mashuzi na mkojo ni ishara ya namna viongozi wanavyowadhulumu wale wanaojaribu kupinga sera zao. Kijana aliyedaiwa kukojolewa na jogoo alipatwa na ugonjwa wa upumbavu asijue la kufanya. Taswira hii inaonyesha namna viongozi wanavyowadhulumu wananchi wake badala ya kuwasaidia kuendeleza mbele hali zao za maisha.

Mwandishi wa tamthilia hizi pia amemulika mwanamke. Kulingana na taswira ya mwanamke, imebainika kwamba, S.A Mohamed alidhamiria kuleta mwamko mpya kwa msomaji ili aone usawa na umuhimu wa kijinsia. Mwandishi pia anamzindua mwanamke ili aone na adai nyadhifa sawa za uongozi sawa na mwanamume. Utafiti huu umeonyesha jinsi mwandishi anapendekeza hadhi ya mwanamke inayotakikana katika maisha ya leo.

Zaidi ya hayo, S.A Mohamed anahimiza vijana kuwa msitari wa mbele katika kuleta mabadiliko kwenye jamii zao. Umuhimu wa mapinduzi na uvumbuzi wa mbinu mpya zinazohitajika kuleta mabadiliko umeachiwa vijana. Mtolewa anagundua tatizo la wari wa Giningi ni unga wa ndere. Aliona suluhisho hilo kuwa unga wa rutuba ambao aliutumia kuwaelimisha. Vijana katika *Mashetani Wamerudi* walivumbua kuwa umoja wao ni ushindi katika kutetea haki na kuleta mapinduzi. Taswira hii ya vijana inaonyesha kwamba S.A Mohamed, alilenga kuwazindua vijana ili watambue nafasi zao na kamwe wasitarajie mkombozi mwingine wa nafsi zao ila wao wenyewe. Vilevile, anawatolea wito wa kupanua mawazo na kushirikiana badala ya utengano usiowafaidi.

Taswira ya walalahoi na walalaheri inawachorea wasomaji kuhusu athari zinazotokana na tofauti za kitabaka. Imefahamika kwamba baadhi ya vifo vya maskini husababishwa na wengine kutokana na tamaa ya mali na ukosefu wa ubinadamu. Taswira ya utabaka pia inalenga kutoa wito kwa viongozi kuonyesha usawa na haki katika utawala wao. Hadithi ya Bi. Kizee inaonyesha namna viongozi wanavyolewa uongozi na kusahau watawaliwa kwa kujilimbikizia mali. Vijana wanapoamua kukongamana kwenye shina la mbuyu wanavurushwa na askarikanzu na kudaiwa kuwa na njama ya kuibadilisha serikali. Wengi wanateswa kwa kupigwa, kunyongwa, kurushiwa maji yanayowasha na hata vitoa machozi kama anavyofanyiwa kijana aliyekimbiza jogoo katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Inaashiria kwamba mwandishi alidhamiria kusisitiza vitendo vya kiutu kwa binadamu wote bila kuzingatia misingi ya maumbile, rangi au hali ya kiuchumi.

Licha ya hayo, mwandishi ameangazia makazi ya kifahari. Taswira hii inalenga kuwazindua wasomaji kuhusu umuhimu wa haki na usawa. Bwana na Bibiye waliishi kwenye jumba kubwa la kifahari wakiwa tu wawili. Bidhaa na vitu vya bei ghali vilipatikana ndani mwa jumba hilo. S.A Mohamed amesawiri jengo hili kuwa la kiajabu ambapo wananchi walifahamu ukubwa na uzuri wake katika harakati zao za kupigania mapinduzi. Tunaweza kusema kuwa S.A Mohamed alikuwa na lengo la kuondoa itikadi ya kikoloni kuwa ni wale tu watawala walio na uwezo wa kuishi na kufurahia maisha . Wengine wana uwezo pia. Vilevile, mwandishi alitaka kumfichulia msomaji unafiki wa viongozi na kumfungua macho ili aone sababu za kupigania na kudai haki zake.

Utafiti huu pia ulibaini kwamba taswira alizotumia S.A Mohamed zililenga maisha ya Mabepari na Makabwela katika msingi wa Kibepari. Mwandishi ameangazia kwa undani mateso na dhuluma zinazotokana na matokeo ya uongozi wa kibepari ambao unatawala nchi nyingi za Kiafrika ikiwemo nchi ya Kenya. Kwa kufanya hivi, mwandishi anawapa mwamko wasomaji ili wajinasue kutoka kwa hali za maisha ya ukandamizwaji. Hii ni kwa sababu anawapa mwanga wa kutambua hali zao, chanzo cha hali zenyewe na mwongozo wa suluhu ambao ni kuanzisha mapinduzi.

Aidha utafiti huu ulibaini kuwa kuna mambo kadhaa ambayo huenda yalichangia matumizi ya taswira katika tamthilia hizi. Kwanza ni mazingira ya uandishi. Sera ya ukoloni na ukoloni mamboleo ilionekana kumwathiri mwandishi kwa sababu ilitawala

sana katika nchi nyingi za Afrika. Hali hii ilionekana kumchukiza mwandishi na kutaka mabadiliko hasa katika siasa. Viongozi waafrika walionekana kuendeleza unyanyasaji dhidi ya Wafrika wenzao hata baada ya mkoloni kuondoka ama kuondolewa. Alitaka wananchi waamke na kupinga uongozi wa kidikteta. Hapa ndipo akaiandika tamthilia ya *Pungwa*. S.A Mohamed hakukomea hapo. Alichukizwa pia na mbinu za kinafiki zilizotumiwa na viongozi kuwakandamiza watawaliwa.Viongozi walijifanya kuwasaidia wananchi huku wakiendeleza mfumo ule ule wa kikoloni katika mbinu zao za kiutawala. Hali hii ilisababisha vifo vya watu wengi waliokuwa msitari wa mbele kupinga sera za serikali. Hata baada ya kuangamizwa kuliendelea kutokea watetezi wengine wa haki na wanaendelea kuibuka. Hapa ndipo akaiandika tamthilia ya *Kivuli Kinaishi.* Hali hii ya ukandamizwaji ilififia kiasi katika nchi nyingi za Afrika katika mwanzo wa karne ya ishirini na moja kutokana na wananchi wengi kupevuka kimawazo na kuendelezwa kwa haki za binadamu. Namna siku zilivyosonga, tunaweza tukadai kwamba mwaandishi alishuhudia mabadiliko ya uongozi na viongozi kadhaa. Kwa kutumia maarifa na ujuzi wa miaka yake ya awali, mwandishi labda ameshuhudia kurejea kwa ukoloni kama sio ukoloni mamboleo. Aliitumia kalamu yake tena kuwazindua wasomaji wake kuhusu uongozi wa kisasa na kuiandika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016).

Utafiti huu unaweza kutoa kauli kwamba misingi ya tamthilia za *Pungwa*, *Kivuli Kinaishi* na *Mashetani Wamerudi* na taswira anazotumia S.A Mohamed ni kioo halisi cha matukio yanayodhihirika katika nchi nyingi za Afrika wakati wa uandishi wake. Tunaweza kusema kuwa Mwandishi ametumia taswira kama silaha ya kupenyeza hisia za ukombozi kwenye akili ya msomaji. Hisia hizi zaonekana kupevua akili za wasomaji na kuchochea hamu ya kutaka mabadiliko ya hali zao. Kupitia matumizi haya bora ya lugha, ujumbe unamfikia msomaji kwa njia aliyoitaka yeye mwenyewe kama vile nadharia ya Umitindo inavyoshikilia. Pia, matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa, S.A Mohamed amekuza matumizi ya taswira zaidi kuliko mbinu nyingine yoyote ile ya lugha.

## 4.3 Hitimisho

Kwa muhtasari, matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwa taswira ni mbinu iliyotumiwa vyema na mwandishi kupitisha ujumbe wake. Utafiti huu pia umeonyesha kuwa licha ya taswira zinazoonekana kama mtindo wa mwandishi wa kupitisha ujumbe, mwandishi pia ametumia tamathali zingine za lugha ambazo kwa kiasi kikubwa zimeelekea kuunda taswira fulani.

Kwa kutathmini matumizi ya taswira katika mtazamo wa umitindo, tamthilia za *Pungwa, Kivuli Kinaishi* na *Mashetani Wamerudi* zinaonekana kuwa kielelezo cha mtindo wa mtu wa kuteua na kutumia lugha. Kwa hivyo, utafiti huu umebainisha taswira kama mbinu ya lugha inayoweza kutumiwa kubainisha tamthilia za S.A Mohamed.

## 4.4 Mapendekezo ya utafiti zaidi

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, tunapendekeza kwamba utafiti zaidi ufanywe kuonyesha matumizi ya mbinu zingine zinazoweza kutumiwa kupitisha ujumbe mzito kwa hadhira lengwa kama vile methali, jazanda, tasifida, kinaya, dhihaka, tashihisi na mbinu zingine.

Aidha utafiti unaweza ukafanywa kuhusu matumizi ya taswira katika riwaya za S.A Mohamed zikiwemo: *Asali Chungu* (1978), *Dunia Mti Mkavu* (1980) miongoni mwa zingine.

# MAREJELEO


Arege, T.M (2015). *Majira ya Utasa*. Nairobi: Spotlight Publishers.

Coser, L. (1963). *Sociology Through Literature : An Introductory Reader*. London: Prentice Hall.

Chapman, R. (1982). *The Language of English Literature*. London: Edward Arnold Publishers Ltd.

Crystal, D. na Davy D. (1969). *Investigating English Style*. London: Longman.

Enkvist, N.E (1992). *Linguistic and Style*. London: Oxford University Press.

Gibbe, A.G. na Mwansoko, D.L. (1971). *Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Hough, G. (1966). *An Essay on Criticism*. Great Britain: Redwood Pron Ltd.

Indangasi, H. (1998). *Stylistics.* Nairobi: Nairobi University Press.

Jakobson, R. (1960). " Linguistics and Poetics", Thomas A. Sebeok (mh) *Style in Language*, Cambridge: MIT Press.

Khatibu, M. (1999). *Tamathali za Semi za Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kitali, M. (2011). Fani na Usawiri wa Kike Katika Tamthilia za *Pango* na *Mama Ee*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Kitsao, J. (1975). A Stylistic Approach for the Study of Written Swahili Prose Texts. Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi.(Haijachapishwa).

Kithaka wa Mberia (1997). *Natala.* Nairobi: Marimba Publication Limited.

Leech, G.N. na Short, M. (1981). *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose.* Nairobi: Longman Group Ltd.

Leech, G.N (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman Group Ltd.

Ligembe, N.E.G (1995). The Uses of Metaphors in Peninah Muhando's *Lina Ubani*. A Stylistic Analysis. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Magare, F.A. (2002). Uhakiki wa Tamthilia ya *Amezidi* kama Kazi ya Kiubwege. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Mbatiah, M. (2014). *Wimbo Mpya.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Mbuthia , E.M. ( 2005 ). A stylistic and Thematic Analysis of Kiswahili Short Stories. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Miriji, T. (1991). Mtindo katika Pungwa ni Hatua Katika Uwasilishaji Ujumbe. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Mirikau, S.A. (2011). Taswira ya Mwanamke Katika Tamthilia za Wamitila K.W. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Mohamed, S.K. (1986 ). *Tamathali za Semi za Kiswahili* Katika *Mulika* Nambari 18. Uk.1-6 Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Mohamed, S.A. (1980). *Utengano.* Longhorn Publishers: Nairobi.

__________ (1988 ). *Pungwa*. Longhorn Kenya Ltd: Nairobi.

__________ (mh) (2010). *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Moran Publishers.

__________ (2016). *Mashetani Wamerudi*. Nairobi: Spotlight Publishers.

__________ (1995). *Amezidi*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

__________ (1995). *Mtindo katika Kunga za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mohamed, M.S. (1978). *Kicheko Cha Ushindi*. Nairobi: Shungwaya Publishers.

Momanyi, C. (1991). Taswira kama Kielelezo cha Uhalisi Katika *Utenzi wa Al-Inkishafi.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Msokile, M. (1993). *Msingi wa Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.

Mtobwa, R.B . (1993). *Najisikia Kuua Tena.* Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Mulokozi, M.M na Kahigi K.K (1973). *Mashairi ya Kisasa.* Dar- es- salaam: Tanzania Publishing House.

Mukobwa, M. (1985). Maendeleo ya Kimaudhui katika Tamthilia Tano za Ebrahim Hussein. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Murungi, K. G (2013). Jinsi Mtindo Unavyoendeleza Maudhui Katika Tamthilia ya *Natala.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Murray, P. (1978). *Literary Criticism: A Glossary of Major Terms*. Newyork: Longman Ltd.

Musembi, N. (2008). Matumizi ya Taswira na Ukinzano kama Kichocheo cha Zinduko katika Riwaya *za G.K Mkangi*: *Mafuta* na *Walenisi*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Musyoka, F.M. (1996). Uhakiki wa Fani Katika Tamthilia za Jay Kitsao. Tasnifu ya Uzamili,Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Mwangi, D.K. (2005). Uhakiki wa Fani Katika Tamthilia za K.W. Wamitila.Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Ngunjiri, D.M. (2012). Matumizi ya Taswira kama Kigezo cha Kufanikisha Maudhui katika Utendi wa Siraji. Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Nguta, M. (2011). Fani na Usawiri na Usawiri wa Kike katika Tamthilia za Pango na Mama Ee. Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Jomo Kenyatta Foundation: Nairobi.

Njogu, S.K. (1987). Maudhui ya Mapinduzi katika Riwaya za Visiwani. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Nyanchama, M.B. (2004). Matumizi ya Taswira na Ishara katika *Sauti ya Dhiki*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Ongarora, S. (2007). *Mtindo katika Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Osiemo, D.O. (1997). Fani katika Ushairi wa Mwalimu Mbega. Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuu Cha Nairobi (Haijachapishwa).

Orwel, G. (1989). *Shamba la Wanyama.* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Plekhanov, G. V. (1957). *Art and Social Life*. Moscow:Progress Publishers Ltd.

Sanja, L. (2014). *Yasinya.* Nairobi: Focus Publishers.

Sarara, M.M (1997). Maudhui katika Tamthilia za S.A Mohamed. Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Senkoro, F.E.M (1987*). Fasihi ya Jamii*. Dar-es-salaam:Press and Publicity.

Shafi, A. (2011). *Mbali na Nyumbani*. Nairobi:Longman Ltd.

Simpson, P. (2004). *Stylistics:* A *resource Book for Students*. London: Routledge.

TUKI (2006). *Kamusi ya Kiingereza – Kiswahili*. Toleo la Tatu: Dar es Salaam:Tuki.

Wamitila, K.W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*: Nairobi: Focuss books.

__________ (2008). *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide – Muwa Publishers Ltd.

__________ (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers Ltd:

Wellek, R. na Warren, A. (1965). *Theory of Literature*. Harcourt: Penguin Books.